

**ISSN 0856 – 034X**

**Supplement No. 18**

**9<sup>th</sup> May, 2014**

**SUBSIDIARY LEGISLATION**

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 19 Vol 95 dated 9<sup>th</sup> May, 2014*

Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of Government

TAARIFA YA SERIKALI NA. 134 la tarehe 09/05/2014

**TAFSIRI YA SHERIA YA MTOTO**  
[SURA YA 13]

TOLEO LA MWAKA, 2014

Toleo hili la Tafsiri ya Sheria ya Mtoto Sura ya 13 ni Tafsiri rasmi ya Kiswahili iliyosanifiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuchapishwa kwa ajili ya kutumiwa na umma kwa kuzingatia kifungu cha 84 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Mbalimbali Sura ya 1. Itokeapo mkanganyiko wowote katika Tafsiri hii ya Kiswahili Toleo lililopitishwa na Bunge kwa lugha ya Kingereza ndilo litakalotumika.

Dar es Salaam,  
6 mei, 2014

FREDERICK M. WEREMA,  
*Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

*Sheria ya Mtoto*

*Tangazo la Serikali Na. 134 (linaendelea)*

**SHERIA YA MTOTO, 2009**

**MPANGILIO WA VIFUNGU**

*Sehemu Kifungu*

**SEHEMU YA KWANZA  
UTANGULIZI**

1. Jina na tarehe ya kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

**SEHEMU YA PILI  
HAKI NA USTAWI WA MTOTO  
(a) Haki ya mtoto**

4. Maana ya “mtoto”.
5. Kutokuwa na ubaguzi.
6. Haki ya jina na utaifa.
7. Haki ya kuishi na wazazi.
8. Wajibu wa kumlea mtoto.
9. Wajibu na majukumu ya mzazi.
10. Haki ya mali ya wazazi
11. Haki ya maoni.
12. Ajira yenye madhara.
13. Kinga dhidi ya mateso na udhalilishaji.
14. Adhabu kukiuka sheria.

*(b) Wajibu wa jumla wa mtoto*

15. Wajibu na majukumu ya mtoto.

**SEHEMU YA TATU  
MATUNZO NA ULINZI WA MTOTO**

16. Maana ya Matunzo na ulinzi wa mtoto na vigezo vya amri ya Matunzo.
17. Matunzo wa mtoto.
18. Amri ya malezi ya Mahakama iwe kwa faida ya mtoto.
19. Usimamizi wa amri ya mahakama ya matunzo iwe ya manufaa kwa mtoto.
20. Majukumu ya Afisa Ustawi wa Jamii.
21. Kutembelea nyumbani.
22. Masharti ya jumla kuhusu amri.

23. Utoaji wa amri.
24. Amri ya matunzo na uasili.
25. Malengo ya amri ya matunzo.
26. Haki ya mtoto pindi wazazi wanapotengana.

**SEHEMU YA NNE**  
**KUWEKWA KWENYE MATUNZO YA KAMBO**

27. Jukumu la mzazi, mlezi meneja, au mzazi wa kambo.
28. Amri ya kutenganishwa.
29. Kutekelezwa kwa amri ya utengaji.
30. Kosa kumwondoa mtoto bila ruksa.
31. Taarifa ya uchunguzi wa kijamii.
32. Masharti ya malezi ya kambo.
33. Hakuna kutangaza taarifa na picha za mtoto.

**SEHEMU YA TANO**  
**KUWA MZAZI, UANGALIZI, KUFIKIKA NA MATUNZO**

34. Maombi ya kuwa mzazi.
35. Uthibitisho wa kuwa mzazi.
36. Kipimo cha kitabibu.
37. Uangalizi.
38. Kufikia.
39. Kufikiria kuhusu uangalizi au kufikia.
40. Kumtoa mtoto kinyume cha sheria isivyo halali.
41. Wajibu wa kumtunza mtoto.
42. Maombi ya Amri ya kumtunza mtoto.
43. Amri ya matunzo dhidi ya anayetuhumiwa kuwa ni baba mzazi.
44. Kufikiriwa kwa amri ya matunzo.
45. Maombi ya taarifa ya uchunguzi wa kijamii.
46. Mtu anayestahili kusimamia amri ya matunzo.
47. Muda wa amri ya matunzo.
48. Kuendelea kwa amri ya matunzo katika mazingira fulani.
49. Mahakama yaweza kurekebisha au kuondoa amri.
50. Mzazi ambaye mtoto hayuko chiniya uangalizi wake atawezekumfikia mtoto.
51. Makosa chini ya sehemu hii.

**SEHEMU YA SITA**  
**MALEZI YA KAMBO NA KUASILI**

52. Mtu anayeweza kuwa mzazi wa kambo.
53. Masharti ya kumweka mtoto kwenye malezi ya kambo.
54. Uwezo wa kutoa amri ya kuasili.

55. Maombi ya kuasili.
56. Mamlaka ya kutoa amri ya kuasili.
57. Ridhaa ya wazazi na walezi.
58. Ridhaa nyingine.
59. Masharti ya amri ya kuasili.
60. Amri ya mpito.
61. Mtoto kufahamu ameasiliwa.
62. Maombi ya mtu asiye mkazi.
63. Watoto ambao wamewahi kuasiliwa.
64. Matokeo ya kuasili ya haki ya kuwa mzazi.
65. Kurithi mali endapo mzazi amefariki bila kuacha wosia.
66. Mgawanyo wa mali endapo wosia umeachwa.
67. Vifungu vya nyongeza kuhusiana na mgawanyo wa mali kwa wosia na bila wosia.
68. Amri ya kuasili na sheria za jadi.
69. Rejesta ya watoto walioasiliwa.
70. Usajili wa uasili.
71. Marekebisho ya amri na masahihisho ya Rejesta.
72. Katazo la malipo na zawadi katika kuasili.
73. Taarifa ita tolewa endapo mtoto anapelekwa nje ya nchi.
74. Uasili unaofanywa na wageni.
75. Kanuni za kuasili.
76. Mipaka au uchapishaji na matangazo.

**SEHEMU YA SABA**

**AJIRA YA MTOTO**

*(a) Ajira ya mtoto*

77. Haki ya mtoto kufanya kazi.
78. Kukatazwa kwa kazi za kinyonyaji.
79. Kukatazwa kwa kazi za usiku.
80. Kukatazwa kwa kazi za kulazimishwa.
81. Haki ya malipo.
82. Ajira hatarishi.
83. Kukatazwa kwa unyanyasaji wa kingono.
84. Matumizi.
85. Usajili wa watoto katika shughuli za viwandani.
86. Uteklezaji.

*(b) Mafunzo ya ufundi*

87. Haki ya kupata weledi.
88. Umri wa chini kwa mafunzo ya ufundi.

89. Jukumu la fundi mchundo.
90. Makubaliano ya mafunzo ya ufundi.
91. Wajibu wa Mwanagenzi.
92. Kuruhusiwa kwa Mwanagenzi.
93. Usuluhishi wa mgogoro.

**SEHEMU YA NANE**  
**HUDUMA ZA KUMSAIDIA MTOTO TOKA KWENYE**  
**MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA**

94. Wajibu wa Serikali za Mtaa kuwalinda watoto na kukuza maelewano baina ya wazazi na watoto.
95. Wajibu wa kutoa taarifa kuhusu ukiukwaji wa haki za mtoto.
96. Upelelezi wa Idara.

**SEHEMU YA TISA**  
**MTOTO ANAYEKINZANA NA SHERIA**  
*(a) Mahakama ya Watoto*

97. Kuanzishwa kwa Mahakama ya Watoto.
98. Mamlaka ya Mahakama ya Watoto.
99. Utaratibu katika Mahakama ya Watoto.
100. Mwenendo wa kesi katika Mahakama za Watoto.
101. Dhamana kwa mtoto.
102. Kufungamana na watu wazima akiwa mahabusu.
103. Mahakama ya Watoto yaweza kusikiliza kesi zote isipokuwa za mauaji.
104. Watoto wanaweza kuwekwa chini ya uangalizi wa mtu anayefaa au taasisi.
105. Wajibu wa mahakama wa kuelezea shitaka.
106. Mshtakiwa kutakiwa kutoa sababu.
107. Mshitakiwa anaweza kutiwa hatiani kwa kukubali kosa.
108. Kuhudhuria, kusimama kizimbani na kusikilizwa kesi katika mahakama ya watoto.
109. Kuhojiwa na upande kinzani shahidi.
110. Utetezi.
111. Utaratibu baada ya kutiwa hatiani.
112. Wazazi wa mtoto aliyeshtakiwa kuhudhuria mahakamani.
113. Uamuizi kuhusu umri.
114. Watu wanaoonekana kuwa na umri wa miaka kumi na nane au zaidi.

*(b) Mtoto kama shahidi*

115. Shahidi Mtoto.

*(c) Hukumu ya kuwa chini ya uangalizi*

116. Amri ya kuwekwa chini ya uangalizi.
117. Masharti pale ambapo mtoto atashindwa kuzingatia masharti ya kuachiliwa.
118. Mamlaka ya kumwamuru mzazi kulipa faini badala ya mtoto.
119. Katazo la adhabu ya kuwekwa chini ya uangalizi na adhabu mbadala.

*(d) Adhabu mbadala*

120. Wakati ambao amri ya kupelekwa katika shule ya maadilisho inaweza kutolewa.

SEHEMU YA KUMI  
SHULE ZA MAADILISHO

121. Shule zilizoidhinishwa.
122. Uteuzi wa Bodi ya wageni.
123. Mamlaka ya Bodi.
124. Amri za Shule zilizoidhinishwa.
125. Kusimamishwa kwa amri ya shule zilizoidhinishwa.
126. Mamlaka ya kuweka kizuizini.
127. Kuongeza muda wa kuwa kizuizini.
128. Mamlaka ya meneja kuwfikisha mahakamani watu waliopo kizuizini.
129. Kuachiliwa au kuhamishwa kutoka katika shule zilizoidhinishwa.
130. Muda wa rufaa.
131. Amri ya Shule iliyoidhinishwa kuanza kutumika wakati uamuzi wa Mahakama Kuu unasubiriwa.
132. Mamlaka ya kutunga kanuni.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

MATUNZO YA KITAASISI

*(a) Makao yaliyothibitishwa au Taasisi*

133. Uidhinishaji wa makazi yaliyothibitishwa.
134. Ufutiliaji wa makao na taasisi.
135. Mamlaka ya Kamishna kutoa maelekezo kwa makao.
136. Ukaguzi wa makao yaliyothibitishwa.
137. Kupokelewa kwa watoto katika makao yaliyothibitishwa.
138. Jukumu la ulezzi kwa wafanyakazi wa makao yaliyothibitishwa.
139. Uwezo wa mahakama kuamuru uchangiaji.
140. Kufutwa kwa leseni ya makao yaliyothibitishwa.

141. Haki ya kusikilizwa.
142. Sababu ya maamuzi kutolewa.
143. Makazi yaliyothibitishwa na uasili.
144. Mama aliye gerezani pamoja na mtoto.
145. Waziri kutunga kanuni za makazi.
146. Makosa na adhabu.

*(b) Vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na  
vituo vya kulelea watoto wachanga*

147. Maombi ya kuendesha kituo cha kulelea watoto wadogo mchana na vituo vya kulelea watoto wachanga.
148. Katazo la baadhi ya watu kuendesha vituo vya kulelea watoto mchana au vituo vya kulelea watoto wachanga.
149. Usajili wa wamiliki kwa vituo.
150. Rejestya ya kituo cha kulelea watoto wadogo mchana na kituo cha kulelea watoto wachanga.
151. Idara ya ukaguzi.

**SEHEMU YA KUMI NA MBILI**  
**MASHARTI MENGINEYO**

152. Sheria ndogo na miongozo.
153. Maelekezo.
154. Waendeshaji waliopo.
155. Makosa na adhabu.
156. Rufaa.
157. Kanuni.
158. Katazo la jumla.
159. Adhabu ya jumla.
160. Kufutwa na masharti yanayoendelea.

**SEHEMU YA KUMI NA TATU**  
**MAREKEBISHO YATOKANAYO**  
*(a) Sehemu Ndogo ya Kwanza*

161. Tafsiri Sura 29.
162. Marekebisho ya kifungu cha 2.
163. Marekebisho ya kifungu cha 17.
164. Marekebisho ya kifungu cha 34.
165. Marekebisho ya kifungu cha 64.
166. Marekebisho ya kifungu cha 67.

*(b) Sehemu Ndogo ya Pili*

167. Tafsiri Sura ya 353.
168. Marekebisho ya kifungu cha 35.
169. Marekebisho ya kifungu cha 59.
170. Marekebisho ya kifungu cha 60.

*(c) Sehemu Ndogo ya Tatu*

171. Tafsiri Sura ya 366.
172. Marekebisho ya kifungu cha 5.

*(d) Sehemu Ndogo ya Nne*

173. Muundo Sura ya 16.
174. Marekebisho ya kifungu cha 1 -15.
175. Marekebisho ya kifungu cha 17.
176. Marekebisho ya kifungu cha 130.
177. Marekebisho ya kifungu cha 131.
178. Marekebisho ya kifungu cha 138.
179. Marekebisho ya kifungu cha 138B.
180. Marekebisho ya kifungu cha 138C.
181. Marekebisho ya kifungu cha 141.
182. Marekebisho ya kifungu cha 142.
183. Marekebisho ya kifungu cha 144.
184. Marekebisho ya kifungu cha 147.
185. Marekebisho ya kifungu cha 154.
186. Marekebisho ya kifungu cha 156.
187. Marekebisho ya kifungu cha 160.
188. Marekebisho ya kifungu cha 166.
189. Marekebisho ya kifungu cha 167.
190. Marekebisho ya kifungu cha 169.
191. Marekebisho ya kifungu cha 245.
192. Marekebisho ya kifungu cha 252.

*(e) Sehemu Ndogo ya Tano*

193. Tafsiri Sura ya 20.
194. Marekebisho ya kifungu cha 188.

---

JEDWALI

---

*Sheria ya Mtoto*

*Tangazo la Serikali Na. 134 (linaendelea)*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SURA YA 13

SHERIA YA MTOTO

Sheria kwa ajili ya kuleta mabadiliko na kuunganisha sheria zote zinazohusu watoto, kuainisha haki za mtoto na kuendeleza na kulinda ustawi wa mtoto kwa lengo la kutekeleza mikataba ya kimataifa na kikanda inayohusu haki za mtoto, malezi ya kambo, uasili na malezi ya mtoto; kuendelea kudhibiti ajira na uanagenzi, na kuweka masharti yanayohusu watoto wanaokinzana na sheria na kuainisha masharti yanayohusiana na hayo.

[1 APRILI, 2010]

Sheria Namba;  
21 ya mwaka, 2009  
Tangazo la Serikali  
Namba 373 la 2011

Tangazo la Serikali Namba 156 la 2010

**SEHEMU YA KWANZA**  
**UTANGULIZI**

Jina na tarehe ya kuanza kutumika	1.-(1) Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009. Kwa taarifa itakayochapishwa kwenye Gazeti la Serikali ataiteua.
Matumizi	2. Sheria hii itatumika Tanzania Bara kwa masuala yanayohusu uendelezaji, ulinzi na utunzaji wa ustawi na haki za mtoto.
Tafsiri	<p>3. Katika Sheria hii, isipokuwa kama mukhtadha utahitaji vinginevyo-</p> <p>“makazi yaliyothibitishwa” maana yake ni makazi yaliyopewa leseni ambamo mtoto hupewa malezi ya kifamilia ya muda;</p> <p>“shule iliyoidhinishwa” maana yake ni shule iliyanzishwa chini ya Sheria hii na inajumuisha eneo lolote au taasisi iliyotangazwa hivyo chini ya masharti ya sheria hii;</p> <p>“elimu ya msingi” maana yake ni elimu rasmi inayotolewa kwa mtoto katika kiwango ambacho kinaweza kuainishwa kulingana na wakati;</p> <p>“unyanyasaji wa mtoto” maana yake ni ukiukwaji wa haki ya mtoto ambao unasababisha madhara ya kimwili, kimaadili, au kifikra ikijumuisha kupigwa, kutukanwa, kubaguliwa, kutelekezwa, kunyanyaswa kijinsia na kazi za kinyonyaji;</p> <p>“maendeleo ya mtoto” kuhusiana na ustawi wa mtoto, ina maana ni mchakato wa mabadiliko ambao kwao mtoto anaweza kujitawala kimwili, kiakili, kihisia na uwezo wa kipaji katika kumwendeleza katika kila nyanja na kumwezesha kukabiliana na mazingira;</p> <p>“mtoto mwenye ulemavu” maana yake ni mtoto mwenye matatizo ya muda mrefu au ya kudumu kimwili, kiakili au kihisia ambayo unamfanya ashindwe na kuzuia ushiriki wake kikamilifu sawa na wenzake;</p> <p>“Kamishna” ina maaa ya Kamishna wa Ustawi wa Jamii;</p> <p>“mahakama” maana yake ni-</p> <ul style="list-style-type: none"><li>(a) Mahakama ya Mwanzo, Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Hakimu Mkazi au Mahakama Kuu;</li><li>(b) kwa madhumuni ya uasili Mahakama Kuu; na</li><li>(c) kwa madhumuni ya malezi – Mahakama ya Watoto;</li></ul> <p>“fundi mchundo” ina maana ya mtu anayefundisha na kutoa maelekezo kwa mwanagenzi katika fani;</p> <p>“kituo cha kulelea watoto wachanga” ina maana sehemu iliyosajiliwa kwa ajili ya maendeleo ya awali ya mtoto kwa madhumuni ya</p>

- kuwapokea na kuwatunza watoto walio chini ya miaka mitano kwa idadi isiyozidi kumi wakati wa mchana au muda mwingine wa siku kwa malipo au bila malipo;
- “kituo cha kulelea watoto mchana” maana yake sehemu iliyosajiliwa kwa ajili ya maendeleo ya awali ya mtoto kwa madhumuni ya kuwapokea na kuwatunza watoto walio chini ya umri wa miaka mitano ikijumuisha kituo cha kulelea watoto wachanga wakati wa mchana au muda mwingine wa siku kwa malipo au bila malipo;
- Sura ya 389 “fukara” itakuwa na maana kama ilivyoelezwa chini ya Sheria ya Omba Omba;
- Sura ya 287 “Wilaya” itakuwa na maana iliyopewa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji);
- Sura ya 288 “familia” maana yake ya baba na mama, mlezi na watoto walioasiliwa au ndugu wa damu na ndugu wa karibu ambayo itawajumuisha babu, bibi, mjomba, shangazi, binamu, mpwa na wanaoishi kwenye nyumba moja;
- “mtu anayefaa” maana yake ya mtu mzima mwenye maadili, hekima na akili timamu ambaye siyo ndugu wa mtoto na ana uwezo wa kumtunza mtoto na amethibitishwa na Afisa Ustawi wa Jamii kuwa na uwezo wa kutoa malezi;
- “malezi au ulezi wa kambo” ina maana mipango ya muda inayofanywa kwa hiari na familia na mtu ambaye hana uhusiano na mtoto kutoa malezi na ulinzi kwa mtoto;
- “mlezi” maana yake ni mtu mwenye mamlaka au uwezo juu ya mtoto au mtu aliyeteuliwa kwa kiapo, wosia au amri ya mahakama kuchukua jukumu la malezi na usimamizi wa mali na haki za mtoto;
- “kazi hatarishi” maana yake kazi yoyote inayomuweka mtoto katika hatari ya kupata madhara ya kimwili au kiakili;
- “nyumba” inapohusu mtoto, ina maana ni mahali ambapo kwa kuzingatia maoni ya mahakama kwa shauri lolote linalohusu mtoto, mzazi au mlezi wa mtoto mwenye makazi ya kudumu yanayofahamika, pale ambapo hakuna mzazi au mlezi aliye hai, makazi ya mwisho ya kudumu ya mzazi au mlezi isipokuwa-
- (a) katika hali ambayo mzazi au mlezi ana makazi ya kudumu zaidi ya yale ya mwanzo, itachukuliwa kuwa alishi au alikuwa anaishi katika makazi yale ya mwanzo;

(b) pale ambapo mahakama inashindwa kutambua makazi ya mtu huyo atachukuliwa kwa madhumuni ya Sheria hii kuwa na makazi katika eneo la mamlaka ya mtaa ambapo mtoto amekutwa;

“taasisi” maana yake makao yaliyothibitishwa, mahabusu ya watoto, shule za maadilisho au taasisi ya watoto walioathirika kijamii na watoto wanaoishi mtaani na itajumuisha mtu au taasisi inayotoa malezi na uangalizi kwa mtoto;

“mahakama ya watoto” maana yake mahakama iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 97;

“Waziri” maana yake Waziri mwenye dhamana na masuala ya watoto;

“mwakilishi” maana yake ni mtu anayeingilia kati kumsaidia mtoto katika maswala ya kisheria na itajumuisha msimamizi wa watoto; *adem item*

Sura ya 56 “Shirika Lisilokuwa la Kiserikali” litakuwa na maana iliyopewa chini ya Sheria ya Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali;

“yatima” maana yake ni mtoto ambaye amefiwa na mzazi mmoja au wote;

“mzazi” maana yake baba au mama mzazi, aliyeasili na mtu mwingine yejote mwenye jukumu la kumlea mtoto;

“Msajili Mkuu” maana yake ni Msajili Mkuu wa vizazi na vifo aliyeteuliwa kwa mujibu na masharti ya Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo;

“mahabusi ya watoto” maana yake ni mahali ambapo mtoto anapata hifadhi salama wakati shauri lake linashughulikiwa;

“ndugu” maana yake ni babu, bibi, kaka, dada, binamu, mjomba, shangazi au mtu yejote katika familia tanda;

“afisa ustawi wa jamii” maana yake ni afisa ustawi wa jamii aliye katika utumishi wa Umma;

“ujira wa chini wa kisekta” maana yake ni malipo ya chini ya ujira yanayowekwa na bodi ya mishahara ya kisekta kwa sekta husika kwa mujibu wa kifungu cha 39 cha Sheria ya Taasisi za Kazi.

Sura ya 300

#### SEHEMU YA PILI

#### HAKI NA USTAWI WA MTOTO

##### (a) *Haki ya mtoto*

Tafsiri ya  
“mtoto”

4.-(1) Mtu yejote mwenye umri chini ya miaka kumi na nane atajulikama kama mtoto.

(2) Maslahi ya mtoto yatakuwa ndiyo msingi wa kuzingatiwa katika masuala yote yanayohusiana na mtoto aidha yatakuwa

yanashughulikiwa na taasisi za umma au taasisi za binafsi za ustawi wa jamii, mahakama au mamlaka za kiutawala.

Kutokuwa  
baguzi

5.-(1) Mtoto atakuwa na haki ya kuishi kwa uhuru bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

(2) Mtu hatambagua mtoto kwa misingi ya jinsia, tabaka, umri, dini, lugha, maoni ya kisiasa, ulemavu, hali ya kiafya, mila, kabilia, uasili wa mjini au kijijini, kuzaliwa, hali ya kijamii na kiuchumi, ukimbizi au kwa misingi mingine.

Haki ya jina  
na utaifa

6.-(1) Mtoto atakuwa na haki ya jina, utaifa na kuwafahamu wazazi wake wa kumzaa na ndugu wengine wa familia tanda.

(2) Mtu hatamyima mtoto haki yake ya jina, utaifa na kufahamu wazazi wake wa kumzaa na ndugu zake wengine kwa kuzingatia masharti ya sheria nyininge.

(3) Kila mzazi au mlezi atakuwa na wajibu wa kusajili kuzaliwa kwa mtoto wake kwa Msajili Mkuu.

Haki ya  
kukua

7.-(1) Mtoto atakuwa na haki ya kuishi na wazazi wake au walezi.

(2) Mtu hatazuia haki ya mtoto ya kuishi na wazazi wake, mlezi na familia tanda na kukua katika mazingira salama isipokuwa kama itaamuliwa na mahakama kwamba kwa kuishi na wazazi au familia-

- (a) kutasababisha madhara kwa mtoto;
- (b) kutomfanya mtoto apate manyanyaso makubwa; au
- (c) hakuwa na maslahi ya mtoto.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (3) na (2), pale ambapo mamlaka yenye uhali au mahakama imeamua kwa mujibu wa sheria na taratibu husika kwamba ni kwa masilahi ya mtoto kumtenganisha kutoka kwa wazazi wake, matunzo bora mbadala yaliyopo yatatolewa kwa mtoto.

Wajibu wa  
kumlea  
mtoto

8.-(1) Itakuwa ni wajibu wa mzazi, mlezi au mtu mwengine ye yeyote anayemlea mtoto kumtunza mtoto huyo na jukumu hilo linampa mtoto haki ya-

- (a) chakula;
- (b) malazi;
- (c) mavazi;
- (d) huduma ya afya pamoja na kinga;
- (e) elimu na muongozo;
- (f) uhuru, na
- (g) haki ya kucheza na kupumzika.

(2) Mtu hatamnyang'anya mtoto haki ya kupata elimu, kinga, chakula, mavazi, malazi, huduma za afya au kitu chochote kinachohitajika kwa ajili ya maendeleo yake.

(3) Mtu hatamnyima mtoto haki ya huduma ya afya kwa sababu ya kidini au imani nyingine.

(4) Mtu hatamnyima mtoto haki ya kushiriki katika michezo, au katika shughuli chanya za kiutamaduni na kisanii au katika shughuli nyingine za starehe isipokuwa kama kwa maoni ya mzazi, mlezi au ushiriki wa mtoto katika shughuli hizo si kwa maslahi yake.

(5) Mtu hatamtendea mtoto mwenye ulemavu kwa namna ambayo si ya kiutu.

(6) Mtoto mwenye ulemavu atastahili uangalizi maalum, matibabu na huduma nafuu kwa ajili ya kumrekebisha na kupata fursa sawa katika elimu na mafunzo kwa kadri itakavyowezekana ili kuendeleza kipaji chake, uwezo wake na kuweza kujitegemea.

Wajibu na  
majukumu  
ya mzazi

9.-(1) Mtoto atakuwa na haki ya kuishi, utu, heshima, mapumziko, uhuru, huduma za afya, elimu na malazi toka kwa wazazi wake.

(2) Haki ya mtoto kupumzika na kuwa huru itazingatia mwongozo na uwezo wa mzazi, mlezi au ndugu.

(3) Kila mzazi atakuwa na wajibu na majukumu yaliyowekwa ama na sheria au vinginevyo kwa mtoto wake ambayo yatajumuisha wajibu wa-

(a) kumlinda mtoto dhidi ya utelekezwaji, ubaguzi, vurugu, unyanyasaji, madhara ya kimwili na kiakili na ukandamizaji;

(b) kutoa mwongozo malezi, msaada na matunzo kwa mtoto na kuhakikisha uhakika wa mtoto kuishi na maendeleo "kuendelezwa"; na

(c) kuhakikisha kuwa kwa muda ambao mzazi hatakuwepo, mtoto atapata malezi toka kwa mtu anayefaa, isipokuwa tu pale ambapo mzazi amekabidhi haki na wajibu huo kwa mtu mwagine kulingana na sheria au kwa taratibu za kimila.

(4) Endapo wazazi wa mtoto wamefariki, jukumu la kumlea linaweza kuhamishiwa kwa ndugu au mlezi aliyeteuliwa kwa amri ya

mahakama au kwa taratibu za kimila.

Haki kwa  
mali za  
wazazi

10. Mtu hatamnyang'anya mtoto haki ya kufaidia ipasavyo mali za wazazi.

Haki ya  
kutoa maoni

11. Mtoto atakuwa na haki ya kutoa maoni na mtu yejote hatamnyima mtoto mwenye uwezo wa kutoa maoni haki ya maoni, ya kusikilizwa na kushiriki katika maamuzi yatakayohusu maisha yake.

Ajira zenye  
madhara

12. Mtu hatamuajiri au kumfanyisha mtoto kazi ambazo zinaweza kuwa na madhara kwa afya, elimu, akili, mwili au kwa maendeleo ya kimaadili ya mtoto.

Ulinzi dhidi  
ya mateso na  
udhalilishaji

13.-(1) Mtu hatamsababishia mtoto mateso, au aina nyingine ya ukatili, kumpa adhabu zisizo za kibinadamu au kumdhailisha mtoto ikijumuisha mila na desturi zozote zenye madhara kwa mtoto kimwili au kiakili.

(2) Adhabu haitakuwa stahili kwa mtoto iwapo ni mbaya kwa aina yake au ni kubwa kwa kiwango chake kulingana na umri wa mtoto, hali ya mtoto kimwili na kiakili; na adhabu haitakuwa stahili kwa mtoto iwapo kutokana na umri mdogo wa mtoto au kwa sababu nyingine hawezi kuelewa lengo la adhabu hiyo.

(3) Istilahi "udhalilishaji" kama ilivyotumika katika kifungu hiki maana yake kitendo kinachofanywa kwa mtoto kwa nia au dhamira ya kumdhailisha au kushusha hadhi yake.

Adhabu

14. Mtu atakayekiuka kifungu chochote katika Sehemu hii atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atalipa faini isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo cha miezi isiyozidi sita au vyote kwa pamoja.

*(b) Wajibu wa jumla wa mtoto*

Wajibu na  
majukumu  
ya mtoto

15. Bila ya kujali masharti yoyote ya Sheria hii, mtoto atakuwa na wajibu na majukumu ya -

- (a) kufanya kazi kwa ajili ya mshikamano wa familia;
- (b) kuwaheshimu wazazi wake, walezi, wakubwa na wazee wakati wote na kuwasaidia pale itakapohitajika;
- (c) kutumikia jamii na taifa lake kwa kutumia uwezo wake

- wa kimwili na kiakili kulingana na umri na uwezo wake;
- (d) kulinda na kuimarisha mshikamano wa kijamii na kitaifa;
- (e) kulinda na kuimarisha tamaduni zisizo na madhara za jamii yake na taifa kwa ujumla kuhusiana na wanajamii wengine au taifa.

**SEHEMU YA TATU  
MATUNZO NA ULINZI WA MTOTO**

Maana ya malezi na ulinzi wa mtoto na vigezo vya amri za malezi

16. Kwa madhumuni ya Sheria hii, mtoto atakuwa anahitaji malezi na ulinzi endapo mtoto huyo -
- (a) ni yatima au ametelekezwa na ndugu zake;
- (b) ametelekezwa au ametendewa visivyo na mtu anayemlea na kumtunza au na mlezi wake au wazazi;
- (c) ana mzazi au mlezi asiyetoa malezi sahihi;
- (d) ni maskini;
- (e) analelewa na mzazi au mlezi ambaye kutokana na tabia za kihalifu au ulevi, hawezi kumlea mtoto;
- (f) ni mzururaji na hana makazi au sehemu ya kuishi;
- (g) ni ombaomba au anaishi kwa kutegemea misaada, ama kwa kisingizio cha kuimba, kucheza, kufanya maonyesho, kuuza kitu chochote au vinginevyo, au anakutwa katika mtaa wowote, jengo, au mahali pengine kwa madhumuni ya kuomba au kupata misaada;
- (h) anaambatana na mtu yejote ambaye anaomba au anayeishi kwa kisingizio cha kuimba kucheza kufanya maonyesho au kuuza kitu chochote au vinginevyo;
- (i) analelewa na mzazi asiye na uwezo au mzazi fukara;
- (j) mara kwa mara anaambatana na mhalifu sugu au kahaba;
- (k) anaishi kwenye nyumba au sehemu ya nyumba inayotumiwa na makahaba kwa lengo la kufanya ukahaba au vinginevyo anaishi katika mazingira yanayosababisha, au kuvutia au kuhamasisha ukahaba au kuathiri maadili ya mtoto;
- (l) ni mtu ambaye kujitia kwake kosa limetendwa au jaribio la kosa chini ya Sheria ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu jaribio limefanywa;
- (m) amekuwa akifanya jambo ambalo kwa namna ambayo inaaminika kuwa anashawishi au amekuwa akishawishi kufanya mambo yaliyo kinyume na maadili;
- (n) yuko chini ya umri unaomfanya awajibike kijinai na

- amehusika kutenda kosa kubwa la jinai;
- (o) kwa namna nyingine, yupo katika mazingira yanayomhatarisha kimaandili au kimwili;
  - (p) analelewa na mtu mwenye ulemavu ambaye ulemavu huo unamfanya asiweze kumpa mtoto malezi stahili;
  - (q) endapo mtoto huyo yupo katika mazingira mengine yoyote kama ambavyo Kamishna ataamua.

Ulinzi wa  
mtoto

17.-(1) Mtu ambaye ni mmiliki au anaendesa au ni msimamizi wa ukumbi wa muziki, baa au klabu ya usiku, hatamruhusu mtoto kuingia katika maeneo hayo.

(2) Mtu hatamuuzia mtoto sigara, pombe, pombe kali, madawa ya kulevyu au kitu chochote kinacholewesha.

(3) Mtu atakayekiuka masharti ya kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na atakapotiba hatiani atalipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi milioni moja na kisichozidi shilingi milioni tano au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na miwili au vyote kwa pamoja.

Amri ya  
malezi ya  
Mahakama  
iwe kwa  
faida ya  
mtoto

18.-(1) Mahakama inaweza, pale ambapo Afisa Ustawi wa Jamii atakapoomba, kutoa amri ya malezi kwa faida ya mtoto.

(2) Amri ya malezi au amri ya muda ya malezi itamtoa mtoto katika mazingira yoyote yanayomdhuru au yanayoweza kumsababishia madhara na kuhamishia haki ya malezi kwa afisa ustawi wa jamii.

(3) Afisa Ustawi wa Jamii atachukua jukumu la kumlea mtoto na ataamua sehemu inayofaa zaidi kwa mtoto ambayo yaweza kuwa-

- (a) makazi yaliyothibitishwa;
- (b) mtu anayefaa;
- (c) mlezi wa kambo aliyeidhinishwa kwa kuzingatia kanuni za malezi ya kambo zilitungwa chini ya Sheria hii; au
- (d) nyumbani kwa mzazi, mlezi au ndugu.

(4) Kipindi cha juu zaidi cha amri ya matunzo kitakuwa ni miaka mitatu au mpaka kipindi ambacho mtoto atakapofikisha umri wa miaka kumi na nane, itategemea kipindi gani kitakuwa mapema zaidi.

(5) Mahakama yaweza kutoa amri nyingine kwamba mzazi, mlezi au mtu mwingine mwenye jukumu la kumlea mtoto kulipa gharama za matunzo ya mtoto.

(6) Mahakama haitamteua meneja au mlezi wa taasisi au makazi yaliyothibitishwa kuwa mtu mwenye uwezo wa kulea aliyethibitishwa ambaye chini yake ulezzi wa mtoto unaweza kuwekwa ni yale ambayo Kamishna, kwa taarifa katika Gazeti la Serikali amethibitisha.

(7) Amri ya matunzo ya muda haitatolewa isipokuwa tu kama mtoto anapata madhara au kuna uwezekano wa mtoto kupata madhara iliyoinishwa katika kifungu cha 16 cha Sheria hii.

Amri ya  
mahakama  
ya usimamizi

19.-(1) Mahakama inaweza, kwa maombi ya Afisa Ustawi wa Jamii ataomba, kutoa amri ya usimamizi au amri ya usimamizi wa muda.

(2) Amri ya usimamizi au usimamizi ya muda italenga kumweka au kumkinga mtoto na madhara yanayosababishwa kwake wakati akiwa katika nyumba ya familia yake chini ya uangalizi wa mzazi wake, mlezi au ndugu.

(3) Amri ya usimamizi ya muda itamweka mtoto chini ya usimamizi wa Afisa Ustawi Jamii au mtu mwingine mwenye uwezo wa kulea katika jamii wakati mtoto akiwa bado yuko chini ya uangalizi wa mzazi wake, mlezi au ndugu.

(4) Kipindi cha juu zaidi cha amri ya usimamizi kitakuwa ni mwaka mmoja au mpaka pale ambapo kutakuwa na maombi ya Afisa Ustawi wa jamii kwa uthibitisho wa Afisa Ustawi wa Jamii pale ambapo kutakuwa na maombi ya Afisa ustawi wa jamii atakapokuwa ameomba.

(5) Kuongeza muda wa amri ya usimamizi kutahitaji taarifa ya maandishi ya Afisa Ustawi wa Jamii.

(6) Amri ya usimamizi itamtaka mtu anayeishi na mtoto -

- (a) kumtaarifu msimamizi mabadiliko yoyote ya anuani yake; na
- (b) kumruhusu msimamizi kumtembelea mtoto nyumbani kwake.

(7) Maombi ya amri ya kumpokea mtoto katika makazi yaliyothibitishwa au taasisi yatakuwa na taarifa zinazohusu-

- (a) jina, umri na anuani ya mtoto;
- (b) jinsi ya mtoto;
- (c) majina ya mzazi, kama yanafahamika;
- (d) utaifa;
- (e) elimu ya mtoto;
- (f) taarifa ya kitabibu kuhusiana na afya ya mtoto;
- (g) mahali alipozaliwa mtoto, kama panafahamika;
- (h) kabilia; na
- (i) dini ya kuzaliwa ya mtoto.

(8) Maombi yatakayofanywa chini ya kifungu hiki yatazingatia-

- (a) maslahi ya mtoto;
- (b) taarifa ya uchunguzi ya Afisa Ustawi Jamii; na
- (c) familia mbadala

Majukumu  
ya Afisa  
Ustawi wa  
Jamii

20. Majukumu ya Afisa Ustawi wa Jamii kuhusiana na malezi au usimamizi wa mtoto ni-

- (a) kumshauri na kumnasihi mtoto na familia yake;
- (b) kufanya mapitio ya mara kwa mara katika mpango wa maendeleo ya mtoto kwa kushauriana na mtoto na wazazi wake au mlezi;
- (c) kuomba mahakama kuondoa au kukubali amri pale itakapolazimu; na
- (d) kuchukua hatua zinazostahili ili kuhakikisha kwamba mtoto hapati madhara.

Kutembelea  
majumbani

21. Afisa Ustawi wa Jamii ataruhusiwa na Mzazi, mlezi au ndugu wa mtoto kumtembelea mtoto katika nyumba ya familia yake au katika makazi yaliyothibitishwa au katika taasisi.

Masharti ya  
jumla ya  
amri

22.-(1) Mtoto atakayekiuka amri ya mahakama na kukimbia anaweza kukamatwa bila hati ya kukamata ya askari polisi, afisa mtendaji wa kijiji, afisa mtendaji wa kata au Afisa Ustawi wa Jamii na kurudishwa katika sehemu ya malezi.

(2) Endapo mtoto atakimbia na mtu mwenye uwezo wa kumlea akakataa kumlea mtoto huyo, mahakama yaweza kutoa amri nyingine ya kumweka mtoto katika shule ya maadilisho.

Utoaji wa  
amri

23. Mahakama inaweza kutoa amri ya matunzo au ya usimamizi kwa maslahi ya mtoto kwa maombi ya-

- (a) mtoto kupitia msimamizi wake;
- (b) Afisa Ustawi wa Jamii;
- (c) askari wa polisi;
- (d) mzazi, mlezi au ndugu wa mtoto; au
- (e) mtu ye yote mwenye jukumu la uzazi.

Amri ya malezi na uasili

24.-(1) Mtoto aliye chini ya amri ya malezi au ya usimamizi ambaye mzazi, mlezi au ndugu yake haonyeshi nia ya kumlea mtoto huyo katika kipindi kilichoamriwa na mahakama, anaweza kuasiliwa na wazazi wa kambo au kulelewa na msimamizi wa makao yaliyothibitishwa .

(2) Maombi ya amri ya ulezi au usimamizi yanaweza kutolewa pale tu -

- (a) njia zote mbadala za kumsaidia mtoto zitakapokuwa zimejaribiwa bila mafanikio;
- (b) madhara anayopata mtoto au madhara anayoweza kupata mtoto yanahitaji mtoto kuondolewa anapoishi; au
- (c) madhara anayopata mtoto ni makubwa kiasi kwamba inalazimu aondolewe haraka kutoka mahali anapoishi.

Dhamira ya amri ya malezi

25.-(1) Dhamira ya amri ya malezi au ya usimamizi ni –

- (a) kumuondoaa mtoto kutoka kwenye mazingira yanayomdhuru au yanayoweza kumdhuru;
- (b) kumsaidia mtoto pamoja na wote waliokuwa wanaoishi na mtoto au wanaotaka kuishi na mtoto;
- (c) kutathmini mazingira yaliyopelekea kutolewa amri hiyo na kuchukua hatua kutatua au kuondoa tatizo ili kuhakikisha kuwa mtoto anarejea kwenye jamii.

(2) Amri ya malezi au ya usimamizi itafanyiwa mapitio angalau mara moja kila mwaka kwa maombi ya Afisa Ustawi wa Jamii.

Haki ya mtoto pindi wazazi wanapo-tengana  
Sura ya 29

26.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Ndoa, pale ambapo wazazi wa mtoto wametengana au kutalakiana, mtoto atakuwa na haki ya-

- (a) matunzo na elimu yenyе ubora ule ule aliyokuwa anaupata kabla wazazi wake hawajatengana au kutalikiana;
- (b) kuishi na mzazi ambaye, kwa maoni ya mahakama, ana uwezo wa kumlea mtoto kwa kuzingatia maslahi ya mtoto; na
- (c) kutembelea na kukaa na mzazi mwingine wakati wowote mtoto atakapotaka isipokuwa kama mpango huo hautaingilia na programu ya masomo au mafunzo.

(2) Kutakuwa na dhana isiyopingika kwamba itakuwa ni kwa maslahi ya mtoto aliye na umri wa chini ya miaka saba kuishi na mama yake isipokuwa katika kuamua kwamba dhana hiyo inafaa kutumika katika shauri husika, mahakama itazingatia kutosumbua maisha ya mtoto kutokana na kubadilisha makaazi yake.

**SEHEMU YA NNE**  
**KUWEKWA KWENYE MALEZI YA KAMBO**

Jukumu la malezi,  
meneja au  
mlezi wa kambo

27.-(1) Mlezi wa makao yaliyothibitishwa au meneja wa taasisi au wazazi wa kambo wanaoishi na mtoto watakuwa na jukumu la uzazi kwa mtoto wakati akiwa chini ya ulezi wake au taasisi.

(2) Mawasiliano kati ya mtoto na wazazi, ndugu au rafiki wakati akiishi kwenye makao yaliyothibitishwa, taasisi au mlezi wa kambo, yatahimizwa isipokuwa tu kama si kwa maslahi ya mtoto.

(3) Mlezi au meneja wa makao yaliyothibitishwa au taasisi au wazazi wa kambo wanaoishi na mtoto watahakikisha kuwa maendeleo ya mtoto wakati akiwa kwenye makao yaliyothibitishwa au taasisi au familia ya kambo hususani afya yake na elimu vinazingatiwa.

(4) Mlezi au meneja wa makao yaliyothibitishwa au taasisi atakuwa na jukumu la kuwasiliana na wazazi au walezi wa mtoto ili kuwajulisha kuhusu maendeleo ya mtoto na kupanga, kupitia kwa Afisa Ustawi wa Jamii, kumrudisha mtoto nyumbani mapema kwa kadri itakavyokuwa inafaa.

(5) Afisa Ustawi wa Jamii atapaswa kumtembelea mtoto nyumbani wakati wa kipindi cha majoribio na kupanga mipango ya maisha ya baadae ya mtoto kwa kushauriana na meneja, mlezi au wazazi wa kambo.

Amri ya  
kutenga

28.-(1) Mahakama ya watoto yaweza, wakati wa kuendesha shauri la maombi ya amri ya malezi, amri ya usimamizi wa muda au amri ya malezi ya muda, kutoa amri ya utengaji inayomzuia mta atakayetajwa katika amri hiyo kuwa na mawasiliano na mtoto pamoja na mta anayemlea mtoto huyo.

(2) Kabla ya kutoa amri ya kutenga, mahakama itajiridhisha kama amri hiyo ni ya lazima kwa ulinzi wa mtoto na kwa kulinda maslahi ya mtoto, au la.

(3) Mahakama yaweza kutaja kipindi cha amri ya utengaji.

Kutekelezwa  
kwa amri ya  
utengaji

29.-(1) Mahakama ya Watoto inaweza kurekebisha au kuondoa amri ya utengaji kwa maombi ya mtu aliyetajwa katika amri hiyo au mtoto husika.

(2) Mahakama yaweza, katika mwenendo wa shauri ya maombi ya amri ya malezi au amri ya usimamizi, kutoa amri ya upekuzi na amri ya kutoa inayomuidhinisha Afisa Ustawi wa Jamii, peke yake au na askari wa polisi, kuingia katika eneo lolote lililoainishwa katika amri na kupekua na kumweka sehemu salama mtoto ye yote ambaye Afisa Ustawi wa Jamii anaamini au anahisi kwamba anadhurika au anaweza kudhurika.

(3) Mtoto aliyeondolewa kuto kana na amri ya mahakama ya upekuzi na ya kutoa, atafikishwa Mahakamani ndani ya siku saba kuanzia siku aliyoondolewa.

(4) Mapema iwezekanavyo na kwa vyovyyote vile ndani ya muda ulioainishwa katika kifungu kidogo cha (3), Afisa Ustawi wa Jamii atampeleka mtoto Mahakamani na atandaa taarifa, kwa kuzingatia matakwa ya mtoto.

(5) Endapo atawekwa chini ya ulinzi wazazi wake, mlezi au watu wengine wanaoishi na mtoto watafahamishwa mapema iwezekanavyo na kuruhusiwa kukutana na mtoto isipokuwa tu kama siyo kwa maslahi ya mtoto.

(6) Mtu ye yote anayekiuka amri ya kutenga anatenda kosa na atakapotija hatihani atalipa faini isiyopungua shilingi laki tano au kifungo kwa muda wa miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

Kosa la  
kumwondo  
mtoto bila  
ruhusa

30.-(1) Mtu ye yote, ambaye bila sababu ya msingi atamtoa au atasababisha mtoto aliye katika ulinzi kuondoka kutoka katika sehemu salama bila ya mamlaka au ruksa ya mtu aliyepeewa dhamana ya kumtunza mtoto, atakuwa ametenda kosa na atakapotija hatiani atalipa faini isiyopungua shilingi laki moja au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

(2) Afisa Ustawi wa Jamii, baada ya kufanya uchunguzi juu ya umuhimu wa kumrudisha mtoto mahali salama, atamrudisha mtoto katika sehemu hiyo ya usalama.

Ripoti ya  
uchunguzi  
wa kijamii

31.-(1) Kabla ya kutoa amri ya malezi au amri ya usimamizi, mahakama itahitaji kupewa taarifa ya uchunguzi wa kijamii kimaandishi kuhusiana na mtoto husika.

(2) Afisa Ustawi wa Jamii atakuwa na wajibu wa kuandaa taarifa ya uchunguzi wa kijamii na atatekeleza amri ya mahakama wakati atakapohitajika kuitoa taarifa hiyo.

(3) Afisa Ustawi wa Jamii atatembelea nyumbani na kuwahoji wazazi, walezi au ndugu wa mtoto husika kabla ya kuandaa taarifa ya uchunguzi wa kijamii.

(4) Endapo mtoto anayehusika na taarifa ya uchunguzi ya kijamii ana umri unaomuwezesha kuelewa, mtoto huyo atahojiwa na Afisa Ustawi wa Jamii.

(5) Taarifa ya uchunguzi wa kijamii itajumuisha masuala yanayohusiana na maslahi ya mtoto na mapendekezo ya hatua zilizopaswa kuchukuliwa na mahakama.

(6) Mahakama itazingatia maelezo yaliyomo kwenye taarifa ya uchunguzi wa kijamii iwapo itahusiana na amri itakayotolewa.

(7) Endapo amri ya mahakama haitatolewa ndani ya siku kumi na nne, mtoto anaweza kuwekwa kwenye makao yaliyothibitishwa au taasisi ikisubiriwa amri ya mahakama ambayo kwa vyovyote vile inapaswa kutolewa ndani ya siku thelathini.

(8) Endapo Mahakama haitaridhika na mapendekezo yaliyotolewa na Afisa Ustawi wa Jamii katika taarifa itaweka kumbukumbu ya sababu za kutokubaliana na mapendekezo hayo.

Masharti ya  
malezi ya  
kambo

32.-(1) Endapo mtoto atakapowekwa kwenye makao yaliyothibitishwa au katika taasisi chini ya amri ya malezi au amri ya usimamizi, Afisa Ustawi wa Jamii, kwa kushirikiana na mlezi au meneja wa makao yaliyothibitishwa au taasisi anaweza kutoa mapendekezo kwa Kamishna kumweka mtoto kwa mtu anayetaka kuwa mzazi wa kambo.

(2) Mtu anayetaka kuwa mzazi wa kambo wa mtoto atapeleka maombi kwa Kamishna wa Ustawi wa Jamii.

(3) Kamishna atakapopokea maombi, atayashughulikia maombi hayo kwa kuzingatia mapendekezo ya Afisa Ustawi wa Jamii, mlezi au meneja.

(4) Endapo Kamishna ataridhika kwamba anayeomba kuwa mzazi wa kambo ni mtu anayeweza kumlea mtoto na kumtunza na vinginevyo akaridhishwa kwamba maslahi ya mtoto kuwekwa katika malezi ya kambo na mwombaji yamezingatiwa, Kamishna ataruhusu mtoto huyo kuwekwa katika malezi hayo ya kambo.

(5) Mlezi wa kambo ambaye amepewa jukumu la kumlea mtoto, atakuwa na jukumu la kumlea mtoto huyo kama vile ni mzazi wa mtoto kwa wakati mtoto atakapokuwa chini ya ulezi wake.

(6) Waziri, kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana na ustawi wa jamii, anaweza kutengeneza kanuni zinazohusu uwekwaji wa mtoto chini ya malezi ya kambo.

Kutokuta-  
ngaza taarifa  
ama picha ya  
mtoto

33.-(1) Mtu hatachapisha taarifa yoyote au piche itakayo-sababisha kumtambua mtoto katika shauri lolote lililoko mahakamani isipokuwa kwa idhini ya mahakama.

(2) Mtu atakayechapisha taarifa yoyote au piche kinyume na kifungu hiki atatenda kosa na atakapotiwa hatiani atalipa faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi milioni kumi na tano au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu au vyote kwa pamoja.

#### SEHEMU YA TANO

MALEZI, UANGALIZI, KUMTEMBELEA MTOTO NA MATUNZO

Maombi ya  
kuwa mzazi

34.-(1) Watu wafuatao wanaweza kuiomba Mahakamani kutoa amri ya kumthibitisha malezi ya mtoto -

- (a) mtoto mwenyewe;
- (b) mzazi wa mtoto;
- (c) mlezi wa mtoto;
- (d) Afisa Ustawi wa Jamii; au
- (e) kwa amri maalum ya mahakama, mtu mwingine yejote.

(2) Maombi katika Mahakama yanaweza kuwasilishwa -

- (a) kabla ya mtoto kuzaliwa;
- (b) baada ya kifo cha baba au mama wa mtoto;
- (c) kabla mtoto hajatimiza umri wa miaka kumi na nane; au kwa kibali maalum cha mahakama baada ya mtoto kutimiza miaka kumi na nane.

- Uthibitisho wa kuwa mzazi Sura ya 29 Sura ya 108 Kipimo cha utabibu

35. Vifuatavyo vitazingatiwa na mahakama kama ushahidi kwa malezi ya mtoto-

(a) ndoa yoyote iliyofungwa kwa kuzingatia Sheria ya Ndoa;

(b) jina la mzazi lililoingizwa kwenye Rejesta ya vizazi na kutunzwa na Msajili Mkuu wa Vizazi;

(c) taratibu za kiasili zilizofanywa na baba wa mtoto;

(d) kutambuliwa na jamii kama mzazi wa mtoto; au

(e) majibu ya Vinasaba vya Binadamu (Human DNA).

36.-(1) Mahakama inaweza kuamuru mtu anayehisiwa kuwa ni mzazi wa mtoto kufanyiwa kipimo cha utatibu na kwa kuzingatia ushahidi ulioko mbele yake, mahakama itatoa amri kwa namna itakavyoona inafaa.

(2) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1), iwapo ushahidi wa mama au ushahidi huru hautapewa nguvu na ushahidi mwengine kwa kiasi cha kuifanya mahakama ijiridhishe, mahakama yaweza, kwa maombi au bila maombi, kuamuru kipimo cha Vinasaba vya Binadamu kifanywe kwa lengo la kumthibitisha baba mzazi wa mtoto.

(3) Mahakama itaamua na kutoa amri ya upande utakaogharamia kipimo cha Vinasaba vya Binadamu.

(4) Endapo Mahakama itatoa amri kuhusiana na baba mzazi wa mtoto, baba huyo mzazi wa mtoto atachukua jukumu la kumtunza mtoto kama vile Mtoto aliyezaliwa ndani ya ndoa, na mtoto huyo, kwa kuzingatia dini ya baba, atakuwa na haki nyingine zote zinazotoka kwa mzazi ikiwemo haki ya kuwa mrithi.

(5) Mtu yeoyote atakayekataa kutekeleza amri ya mahakama iliyotolewa chini ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na atakapotiya hatiani atalipa faini isiyopungua shilingi laki tano au kifungo cha miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

Uangalizi

37.-(1) Mzazi, mlezi au ndugu anayemlea mtoto anaweza kuiomba mahakama impe uangalizi wa mtoto.

(2) Mahakama inaweza, katika shauri hilo hilo la utoaji wa tamko la ulezii kutoa amri ya uangalizi wa mtoto kwa muombaji kwa kuzingatia masharti kama itakavyoona inafaa.

(3) Mahakama inaweza, wakati wowote kutengua amri ya uangalizi kutoka kwa mtu mmoja na kwenda kwa mtu mwingine, makao yaliyothibitishwa au taasisi kama itakavyoona ni lazima.

(4) Katika kufikia maamuzi yake chini ya kifungu kidogo cha (2) au (3), mahakama itazingatia maslahi ya mtoto kwanza.

Kumtembe-  
lea mtoto      38. Mzazi, mlezi au ndugu aliyekuwa anamlea mtoto kabla ya Mahakama kuamuru mtoto huyo alelewe na mtu mwingine, anaweza kuiomba mahakama imruhusu kumtembelea mtoto katika vipindi fulani.

Jambo la  
kuzingatia      39.-(1) Mahakama itazingatia maslahi ya mtoto na umuhimu wa mtoto kukaa na mama yake wakati inapotoa amri ya uangalizi au kumtembelea mtoto.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), Mahakama itazingatia pia-

- (a) haki ya mtoto chini ya kifungu cha 26;
- (b) umri na jinsia ya mtoto;
- (c) kuzingatia kuwa na wazazi wake isipokuwa tu kama haki zake zinavunjwa mara kwa mara na wazazi wake;
- (d) maoni ya mtoto kama maoni hayo yametolewa huru;
- (e) kuwa ni muhimu kuwaweka watoto pamoja;
- (f) kuzingatia umuhimu wa mwendelezo wa malezi na usimamizi wa mtoto; na
- (g) sababu nyingine yoyote ambayo mahakama itaona inafaa.

Kumtoa  
mtoto isivyo  
halali      40. Mtu ye yoyote ambaye atamtoa mtoto kinyume cha sheria kutoka katika uangalizi halali wa mtu mwingine, makazi yaliyothibitishwa au taasisi, atakuwa ametenda kosa.

Wajibu wa  
kumtunza  
mtoto      41. Mzazi ambaye amri ya malezi imetolewa kwake atakuwa na wajibu wa kuchangia ustawi na matunzo ya mtoto na kutoa mahitaji muhimu kwa uhai na maendeleo ya mtoto.

Maombi ya  
Amri ya  
matunzo      42.-(1) Watu wafuatao wanaweza kuiomba mahakama kutoa amri ya matunzo kwa ajili ya mtoto -

- (a) mzazi wa mtoto;
- (b) mlezi wa mtoto;
- (c) mtoto, mwenyewe kupitia mwangalizi wake;
- (d) Afisa Ustawi wa Jamii; au

(e) ndugu wa mtoto.

(2) Maombi ya kumtunza mtoto yanaweza kufanywa dhidi ya mtu yeyote mwenye uwezo wa kumtunza mtoto au kuchangia katika ustawi na matunzo ya mtoto huyo.

Amri ya  
matunzo  
dhidi ya baba  
mzazi

43.-(1) Maombi ya amri ya matunzo yanaweza kufanywa mahakamani dhidi ya mtu anayesadikiwa kuwa ni baba mzazi wa mtoto –

- (a) na mama mtarajiwa, wakati wowote kabla ya mtoto kuzaliwa;
- (b) wakati wowote ndani ya masaa ishirini na nne tangu mtoto alipozaliwa;
- (c) wakati wowote baada ya mtoto kuzaliwa pakiwa na uthibitisho kwamba mtu anayesadikiwa kuwa ni baba mzazi wa mtoto aliwahi kutoa fedha za matunzo ya mtoto ndani ya miezi ishirini na nne baada ya mtoto kuzaliwa;
- (d) katika muda wowote ndani ya miezi ishirini na nne baada ya mtu anayesadikiwa kuwa ni baba mzazi wa mtoto kurudi Tanzania Bara, baada ya kuthibitisha kwamba aliacha kuishi Tanzania Bara kabla au baada ya mtoto kuzaliwa; au
- (e) na mtu ambaye amri ya kuwa mzazi imetolewa na mahakama dhidi yake kulingana na kifungu cha 34 cha Sheria hii.

(2) Mahakama itakataa kutoa amri ya matunzo chini ya kifungu cha (1) isipokuwa kama itaridhika kwamba-

- (a) kuna sababu za msingi za kuamini kwamba mtu anayesadikiwa kuwa ni baba wa mtoto ni baba wa mtoto kweli na kwamba maombi ya amri ya matunzo yamefanywa kwa nia njema na si kwa lengo lolote la kudhalilisha au kumrubuni ; na
- (b) mtu anayesadikiwa kuwa ni baba wa mtoto alishaombwa na mwombaji au mtu mwengine kwa niaba yake, kutoa matunzo ya mtoto na amekuwa akikataa kutoa mtunzo au amekuwa akitoa matunzo yasiyotosheleza.

Mambo ya  
kuzingatia  
wakati wa  
kutoa amri  
ya matunzo

44. Mahakama itazingatia mambo yafuatayo wakati inapotoa amri ya matunzo-

- (a) kipato na utajiri wa wazazi wote wa mtoto na wa mtu ambaye anawajibika kumtunza mtoto kisheria;
- (b) upungufu wowote wa uwezo wa kutafuta kipato wa mtu mwenye jukumu la kumtunza mtoto;
- (c) majukumu ya kifedha ya mtu anayehusika na matunzo kwa watoto wengine;

- (d) gharama za maisha katika eneo ambalo mtoto anaishi;  
(e) haki za mtoto chini ya Sheria hii.

Ombi la  
taarifa ya  
uchunguzi  
wa kijamii

45.-(1) Mahakama yaweza kumuamuru Afisa Ustawi wa Jamii kuandaa taarifa ya uchunguzi wa kijamii kabla ya kutoa uamuji juu ya maombi ya amri ya matunzo, uangalizi na kumtembelea mtoto.

(2) Mahakama katika kutoa amri hizo itazingatia taarifa ya uchunguzi wa kijamii iliyoandaliwa na Afisa Ustawi wa Jamii.

Mtu  
anayestahili  
kusimamia  
amri ya  
matunzo

46.-(1) Mtu yejote anayeishi na mtoto ambaye amri ya matunzo imetolewa kwa ajili yake ana haki ya kupokea na kuisimamia amri ya matunzo iliyotolewa na mahakama.

(2) Endapo mzazi, mlezi au mtu mwingine yejote anayemlea mtoto atakoma kuwa mtu mwenye uwezo wa kulea, mahakama ya eneo analoishi mtoto yaweza kumteua mtu mwingine kumlea mtoto huyo na kusimamia amri ya matunzo na mtu huyo atakuwa kama vile aliyeteuliwa na mahakama toka mwanzo.

Kipindi cha  
amri ya  
matunzo

47. Amri ya matunzo iliyotolewa na mahakama itakwisha nguvu pale ambapo mtoto atakuwa amefikia umri wa miaka kumi na nane, ameajiriwa kwa malipo au atakapofariki kabla ya kufikia umri wa miaka kumi na nane.

Kuendelea  
kwa amri ya  
matunzo  
katika  
mazingira  
fulani

48.-(1) Bila ya kujali masharti ya kifungu cha 47, mahakama inaweza kuendelea kutekeleza amri ya matunzo baada ya mtoto kufikia umri wa miaka kumi na nane iwapo mtoto atakuwa anaendelea na elimu au mafunzo.

(2) Maombi chini ya kifungu hiki yaweza kuletwa na mzazi wa mtoto, mtu yejote anayemlea mtoto au mtoto mwenyewe.

(3) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (2), maombi ya kutekeleza amri ya matunzo yanawenza kuletwa mahakamani na mtu yejote ndani ya siku arobaini na tano baada ya amri kutolewa.

Mahakama  
yaweza  
kurekebisha  
au kuondoa  
amri

49. Mahakama yaweza, kama itaridhika kurekebisha au kuondoa amri ya matunzo kwa maombi ya mzazi, mtu anayemlea mtoto au mtu mwingine yejote aliyeteuliwa kisheria kumlea mtoto.

Mzazi asiye  
na haki ya

50. Mzazi asiye na haki ya uangalizi wa mtoto na ambaye

kumlea  
mtoto ana  
haki ya  
kumuona  
mtoto

maombi ya uzazi, malezi, kumtembelea mtoto au matunzo yameletwa mahakamani dhidi yake atakuwa na haki ya kumuona mtoto aliyekusudiwa katika amri hiyo.

Makosa chini  
ya sehemu  
hii

51. Mtu yeyote ambaye -

- (a) atamtoa mtoto isivyo halali kutoka kwa mtu mwenye uhalali wa kumlea mtoto kinyume cha kifungu cha 37; au
- (b) atashindwa kutoa mahitaji muhimu ya maisha na maendeleo ya mtoto wakati anapaswa kisheria kufanya hivyo chini ya vifungu vya 41 na 46,

anatenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyopungua shilingi laki tano na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka mitatu au vyote kwa pamoja.

**SEHEMU YA SITA  
MALEZI YA KAMBO NA KUASILI**

Mtu  
anayeweza  
kuwa mzazi  
wa kambo

52.-(1) Mtu yeyote mwenye umri unaozidi miaka ishirini na moja, mwenye maadili na uaminifu uliyothibitishwa anaweza kuwa mlezi wa kambo wa mtoto.

(2) “Mlezi wa kambo” kama inavyotumika katika sehemu hii, ina maana yake ni mtu ambaye si mzazi wa mtoto ila ana nia na uwezo wa kumlea mtoto na kumpatia matunzo.

Masharti ya  
kuweka  
mtoto  
kwenye  
malezi ya  
kambo

53.-(1) Endapo-

- (a) mtoto amewekwa katika makao yaliyothibitishwa au katika taasisi chini ya amri ya usimamizi;
- (b) maoni yametolewa na Afisa Ustawi wa Jamii kwamba makao yaliyothibitishwa au taasisi ndiyo sahemu nzuri ya mtoto kuishi; au
- (c) mtoto amewekwa katika makao yaliyothibitishwa au taasisi na mtu yeyote, Kamishna anaweza kumweka mtoto huyo na mlezi wa kambo.

(2) Maombi ya kuwa mlezi wa kambo yatapelekwa kwa Kamishna kupitia kwa Afisa Ustawi wa Jamii, mlezi au kwa msimamizi wa makao yaliyothibitishwa.

(3) Mlezi yeyote wa kambo aliyepewa jukumu la kumlea mtoto atakuwa na jukumu la kumlea mtoto kama vile yeye ndiye mzazi wa mtoto.

(4) Mtoto aliye chini ya malezi ya kambo atakuwa na haki ya kuabudu kulingana na dini yake ya kuzaliwa.

(5) Mlezi yeyote wa kambo atakayekiuka masharti ya Sehemu hii atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria hii.

(6) Waziri mwenye dhamana na ustawi wa jamii, kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana na masuala ya watoto anaweza kutengeneza Kanuni za malezi ya kambo; au

(7) Bila ya kujali masharti yoyote ya kifungu hiki Kamishna anaweza kwa hati, kumweka mtoto yeyote chini ya malezi ya Kambo kwa muda.

Uwezo wa  
kutoa amri  
ya kuasili

54.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii-

- (a) maombi ya amri ya kuasili yatafanywa Mahakama Kuu; na
- (b) maombi ya uasili wa wazi yatafanywa kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi au Mahakama ya Wilaya.

(2) Baada ya kupokea maombi, mahakama yaweza kukubali maombi ya kuasili au ya uasili wa wazi kulingana na Sheria hii.

(3) Istilahi “uasili wa wazi” kama ilivyotumika katika Sheria hii maana yake ni uasili wa mtoto unaofanywa na ndugu.

Maombi ya  
kuasili

55.-(1) Maombi ya amri ya kuasili yanaweza kufanywa kwa pamoja na -

- (a) mume na mke, au
- (b) mama au baba wa mtoto peke yake au kwa pamoja na mwenzi wake.

(2) Kwa suala la uasili wa wazi, maombi ya kuasili yanaweza kufanywa na ndugu.

Masharti ya  
kutoa amri  
ya kuasili

56.-(1) Amri ya kuasili haitatolewa isipokuwa kama mwombaji au, iwapo ni ombi la waombaji wawili, mmoja wa waombaji -

- (a) ana umri unaozidi miaka ishirini na tano na angalau ana umri unaomzidi mtoto kwa miaka ishirini na moja;
- (b) ni ndugu wa mtoto na ana umri wa miaka ishirini na tano au zaidi;
- (c) kwa maombi ya mwanandoa, mwanandoa mwenza ameridhia kuasili huko; au

(d) ni mwanamke ambaye hajaolewa na ni raia wa Tanzania, na kwa kuzingatia maslahi ya mtoto.

(2) Mwombaji ambaye ni mwanaume atakubaliwa kuasili iwapo maombi yatakuwa ni ya kumuasili mtoto wake au mahakama ikiridhika kuwa kuna mazingira ya kipekee yanayopelekea amri kutolewa.

(3) Amri ya kuasili mtoto haitatolewa isipokuwa kama -

- (a) mwombaji na mtoto wanaishi Tanzania ila sharti hili halitatumika iwapo mwombaji ni raia wa Tanzania anayeishi nje ya nchi;
- (b) mtoto amekuwa akiendelea kulelewa na mwombaji angalau kwa kipindi cha miezi sita mfululizo kabla ya tarehe ya kuwasilisha maombi; na
- (c) mwombaji amemtaarifu Kamishna wa ustawi wa jamii kuhusu nia yake ya kuomba amri ya kuasili mtoto angalau miezi mitatu kabla ya tarehe ya amri.

(4) Isipokuwa kama waombaji ni mume na mke au baba na mama, vyovyothe itakavyokuwa, amri ya kuasili haitatolewa kumruhusu mtu zaidi ya mmoja kumuasili mtoto.

Ridhaa ya  
wazazi au  
walezi

57.-(1) Amri ya kuasili itatolewa tu kwa ridhaa ya wazazi au mlezi wa mtoto.

(2) Bila kujali kifungu kidogo cha (1), mahakama inaweza kuachana na kupata ridhaa ridhaa ya mzazi, mlezi au ndugu wa mtoto, endapo itaridhika kwamba-

- (a) mzazi, mlezi au ndugu amemtelekeza au amekuwa akimtesa mtoto;
- (b) mtu huyo hapatikani au hawezikutoa ridhaa au anakataa kutoa ridhaa bila sababu za msingi.

(3) Mzazi, mlezi au ndugu yeyote wa mtoto ambaye ni mlengwa wa maombi ya kuasili au ambaye ametoa ridhaa ya amri ya kuasili hastastahili kumwondoaa mtoto kutoka katika malezi na milki ya mwombaji isipokuwa kwa ruhusa ya mahakama na kwa maslahi ya mtoto.

Ridhaa  
nyingine

58.-(1) Mahakama yaweza kuomba ridhaa ya mtu yeyote kwa ajili ya amri ya kuasili kama ikiona kwamba mtu huyo ana haki yoyote au wajibu unaohusiana na mtoto kwa makubaliano au amri ya mahakama.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 56, iwapo mwanandoa ni mwombaji pekee, mahakama itahitaji ridhaa ya mwenzi wa mtu huyo kabla amri ya kuasili hajatolewa.

(3) Bila kujali masharti ya kifungu hiki, amri ya kuasili haitatolewa kwa mtu aliyetajwa katika kifungu cha 55 kama mtu huyo anaishi katika mahusiano ya ndoa ya jinsia moja au vyovoyote itakavyokuwa.

Masharti ya  
amri ya  
kuasili

59.-(1) Mahakama itatoa amri ya kuasili iwapo itaridhika kuwa

- - (a) ridhaa inayohitajika kwa amri ya kuasili imetolewa na kwamba mzazi au mlezi wa mtoto anaelewa matokeo ya amri ya kuasili inamaanisha kuwa haki ya kuwa mzazi inaondoka kabisa;
  - (b) ni kwa maslahi ya mtoto na matakwa ya mtoto yamezingatiwa iwapo mtoto anaweza kutoa maoni;
  - (c) kama mtoto ana umri angalau wa miaka kumi na nne, ridhaa yake ya kuasiliwa imetolewa, isipokuwa kama mtoto hawezikutoa maoni; na
  - (d) mwombaji hajapokea au hajakubali kupokea malipo yoyote na hakuna mtu yeyote aliyefanya au aliyekubali kufanya malipo yoyote ama aliyetoa au aliyekubali kutoa zawadi kwa mwombaji isipokuwa kwa namna mahakama itakavyoamuru.

(2) Bila kujali kifungu kidogo cha (1), mahakama haitatoa amri ya kuasili isipokuwa kama kuna taarifa ya uchunguzi ya kijamii iliyoandaliwa na Afisa Ustawi wa Jamii ikiunga mkono maombi ya kuasili na mahakama inaweza kuwataka watu wengine au mamlaka ya serikali ya mtaa kutoa taarifa kuhusiana na maombi hayo.

(3) Mahakama yaweza kutoa masharti wakati inapotoa amri ya kuasili na inaweza kumtaka mwombaji aweke dhamana kwa madhumuni hayo kuhusiana na mtoto pale mahakama itakavyoona pana ulazima.

(4) Amri ya kuasili itakuwa na taarifa zifuatazo -

- (a) tarehe na mahali alipozaliwa mtoto;
- (b) jina, jinsia na jina la ukoo wa mtoto kabla na baada ya kuasiliwa;
- (c) jina, jina la ukoo, anuani, mahali pa kuzaliwa, makazi, uraia na kazi ya mzazi anayeasili; na

(d) tarehe ya kutolewa amri ya kuasili.

(5) Amri ya kuasili haitatolewa dhidi ya mtoto yeote isipokuwa kama mtoto huyo amekuwa akitunzwa na kulelewa na mwombaji angalao kwa kipindi cha miezi mitatu mfululizo kabla ya tarehe ya amri.

Amri ya  
muda

60.-(1) Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika kifungu hiki, mahakama yaweza kuahirisha kushughulikia maombi ya kuasili na kutoa amri ya muda ya kumpa mwombaji jukumu la kumlea mtoto kwa kipindi kisichozidi miaka miwili kwa njia ya majoribio na yaweza kutoa masharti mengine ikiwemo kutoa matunzo, elimu na usimamizi wa mtoto kwa namna itakavyoona inafaa.

(2) Mahakama wakati inapotoa amri ya muda, itaweka masharti kwamba mtoto-

- (a) atakuwa chini ya usimamizi wa Afisa Ustawi wa Jamii; na
- (b) hatapelekwa nje ya Tanzania bila ya ruhusa ya mahakama.

(3) Ridhaa na uwezo wa kutohitaji ridhaa wakati wa kutoa amri ya muda itakuwa sawa na wakati wa kutoa amri ya kuasili.

(4) Amri ya muda haitachukuliwa kuwa amri ya kuasili chini ya Sehemu hii.

Mtoto  
kufahamu  
ameasiliwa

61.-(1) Mzazi aliyeasili atamjulisha mtoto aliyeasiliwa kwamba ameasiliwa na atawajulisha wazazi wake isipokuwa kumjulisha huko kutafanywa kama-

- (a) ni kwa maslahi ya mtoto; na
- (b) mtoto ana angalau umri wa miaka kumi na nne.

(2) Mtu yeote ambaye si mzazi aliyeasili mtoto hatoruhusiwa kumjulisha mtoto kuwa ameasiliwa isipokuwa mzazi aliymuasili.

(3) Mtu yeote atakayekiuka kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na atakapotiba hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi milioni mbili au kifugo kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

Maombi ya  
mtu asiyeye  
mkazi

62.-(1) Katika maombi ya kuasili yanayofanywa na mwombaji ambaye ni mtanzania ambaye si mkazi wa Tanzania au iwapo kuna maombi ya pamoja na mwombaji mmojawapo si mkazi wa Tanzania,

mahakama itajiridhisha kwanza kwamba kuna taarifa za kutosha zitakazopelekea kuamua maombi hayo na baadaye itatoa amri ya muda.

(2) Mahakama, kabla ya kutoa amri ya muda au amri ya kuasili, itajiridhisha kuwa kuna taarifa za kutosha zitakazopelekea kuamua maombi kutoka katika mamlaka inayotambulika ya sehemu ambayo mwombaji anaishi kwa muda huo na kutoka katika nchi yake ya asili.

Watoto  
ambao  
wamewahi  
kuasiliwa

63. Amri ya kuasili au amri ya muda yaweza kutolewa kwa ajili ya mtoto ambaye amewahi kuasiliwa na mzazi aliyeasili ambaye ametajwa katika uasili wa mwanzo, kama yuko hai, itachukuliwa kwamba ndiye mzazi au mlezi wa mtoto kwa madhumuni ya uasili unaofuata.

Matokeo ya  
kuasili ya  
haki ya kuwa  
mzazi

64.-(1) Wakati amri ya kuasili inapotolewa-

- (a) haki, wajibu na majukumu ya wazazi wa mtoto au za mtu mwingine ye yeyote anayehusiana na mtoto yakiwemo yale yaliyo chini ya Sheria za Jadi hazitatumika tena; na
- (b) mzazi aliye muasili mtoto atachukuwa jukumu la haki ya kuwa mzazi, wajibu, majukumu na dhima ya mtoto kuhusiana na sehemu ya uangalizi, matunzo na elimu kama vile mtoto alizaliwa na mzazi aliye muasili ndani ya ndoa halali na si mtoto wa mtu mwingine ye yeyote.

(2) Endapo amri ya kuasili imetolewa kwa pamoja kwa mume na mke, wote kwa pamoja, watachukua na jukumu la kuwa wazazi wa mtoto wote kwa pamoja na mtoto atahusiana nao kama wazazi, kama vile walimzaa wakiwa kama mke na mume.

Kurithi mali  
endapo  
mzazi  
amefariki  
bila kuacha  
wosia

65.-(1) Endapo mzazi aliyeasili amefariki bila kuacha wosia, mali zake zitarithiwa kwa taratibu zote kama vile mtoto aliyeasiliwa ni mtoto wa kumzaa wa mzazi aliyeasili.

(2) Kwa kuondoa mashaka, mtoto aliyeasiliwa hatakuwa na haki ya kurithi kwa wazazi wake wa kumzaa iwapo watafariki bila ya kuacha wosia.

Mgawanyo  
wa mali  
endapo

66.-(1) Katika mgawanyo wa mali zinazohamishika au mali binafsi iwapo wosia umeachwa baada ya amri ya kuasili, ama kimaandishi au la-

wosia  
umeachwa

- (a) marejeo yoyote ama ya moja kwa moja au vinginevyo kwa watoto wa mzazi aliyeasili, isipokuwa kama nia tofauti itathibitishwa, yatatafsiriwa kama au yatajumuisha marejeo ya mtoto aliyeasiliwa;
- (b) iwapo mgawanyo wa mali uliofanywa na mzazi aliyeasili kabla ya amri ya kuasili kutolewa haujumuishi mtoto aliyeasiliwa, mtoto aliyeasiliwa anaweza kuiomba mahakama kurekebisha mgawanyo huo ili mtoto aliyeasiliwa naye ajumuishwe kwenye urithi wa mzazi aliyeemuasili;
- (c) Marejeo yoyote katika wosia wa wazazi wa kumzaa mtoto aliyeasiliwa hayatatafsiriwa kumjumuisha mtoto aliyeasiliwa isipokuwa kama nia tofauti itathibitika; na
- (d) Marejeo yoyote kwa mtu mwenye uhusiano na mzazi aliyeasili, iwapo nia tofauti itathibitika, yatatafsiriwa kama vile mtu huyo ni ndugu wa mtoto aliyeasiliwa.
- (2) Mgawanyo wa mali unaotokana na wosia ulioandaliwa kabla ya tarehe iliyotolewa amri ya kuasili hautachukuliwa, kwa madhumuni ya kifungu hiki, kuwa ulifanywa baada ya tarehe ambayo amri ya kuasili ilitolewa kwa kiambatisho cha wosia kinachofanya wosia uanzie nyuma.
- (3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki maneno “mgawanyo wa mali” yana maana ya mgawanyo wa daawa katika mali kwa hati rasmi au *inter vivos* au kwa wosia ikiwemo kiambatisho cha wosia.

Vifungu vya  
nyongeza  
kuhusiana na  
mgawanyo  
wa mali kwa  
wosia na bila  
wosia

67.-(1) Wasimamizi wa mirathi au watekelezaji wa wosia wanaweza kugawa mali za marehemu kwa watu wanaostahili bila kuwajibika kwa lolote.

(2) Iwapo wakati wa mgawanyo wa mali msimamizi au mtekelezaji wa wosia atakuwa hajapata notisi ya amri ya kuasili inayompa stahili mtoto aliyeasiliwa kunufaika na mali ya urithi, mtoto huyo aliyeasiliwa anayestahili atakuwa na haki ya kufuatilia mali hizo kwa yejote isipokuwa kwa mtu aliyenunua kwa nia njema.

Isipokuwa mali hizo hazitauzwa au kuhamishiwa kwa mtu mwininge yejote mpaka pale shauri hilo litakapoamuliwa.

(3) Maombi ya awali ya amri ya kuasili mtoto ambaye ameasiliwa kwa mara ya pili hayatazingatiwa kwa madhumuni ya mgawanyo wa mali baada ya kifo cha mzazi aliyeasili awali.

- Amri ya kuasili na sheria za jadi      68.-(1) Sheria za jadi zitamhusu mtoto aliyeasiliwa kama vile ni mtoto wa kuzaliwa wa mzazi aliyemuasili iwapo tu mzazi aliyemuasili yuko chini ya Sheria za Jadi.
- Rejesta ya watoto walioasiliwa      (2) Endapo kuna kuasili kwa pamoja kati ya mke na mume, marejeo ya mzazi aliyeasili katika kifungu hiki yatachukuliwa kuwa marejeo ya mume na mke.
- Usajili wa uasili      69.-(1) Msajili Mkuu ataweka na kutunza katika ofisi yake Rejesta ya watoto walioasiliwa ambamo ataweka taarifa za amri ya kuasili au amri ya muda iliyotolewa na Mahakama
- (2) Kila amri ya kuasili au amri ya muda iliyotolewa na mahakama itapelekwa kwa Msajili Mkuu na msajili wa Mahakama Kuu ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya amri.
- (3) Msajili Mkuu atahifadhi kumbukumbu nyingine zinahusiana na taarifa katika Rejesta ya vizazi wakati wa kuasili pamoja na taarifa katika Rejesta ya watoto walioasiliwa lakini taarifa hizi hazitakuwa wazi kwa umma au kwa mtu ye yeyote isipokuwa kwa amri ya mahakama.
- 70.-(1) Amri ya kuasili iliyotolewa na mahakama itakuwa na maelekezo yanayomtaka Msajili Mkuu kuingiza taarifa katika Rejesta ya watoto walioasiliwa kwa namna ilivyoainishwa katika Jedwali la Sheria hii.
- (2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (3), itaainisha taarifa zitakazoingizwa katika safu ya 2 mpaka ya 6 ya Jedwali la Sheria hii.
- (3) Kwa ajili ya kutekeleza masharti ya kifungu kidogo cha (1), iwapo-
- (a) tarehe sahihi ya kuzaliwa mtoto haijathibitishwa kwa kiasi cha kuiwezesha mahakama kuridhika, mahakama itaamua tarehe inayoweza kuwa ya kuzaliwa mtoto na tarehe hiyo iliyoamuliwa itakuwa ndiyo tarehe itakayoainishwa kwenye amri;
- (b) jina au jina la ukoo ambalo mtoto atapewa baada ya kuasiliwa linatofautiana na jina la asili au jina la ukoo wa asili, jina jipya au jina jipya la ukoo litaainishwa katika amri badala ya jina la asili; na
- (c) nchi aliyozaliwa mtoto haijathibitishwa kwa kiasi cha kuiridhisha mahakama, taarifa za nchi hiyo, bila kujali

chochote katika kifungu hiki kidogo, zitaondolewa kwenye amri na kwenye taarifa za Rejesta ya watoto walioasiliwa.

(4) Endapo baada ya maombi ya amri ya kuasili mtoto kupelekwa mahakamani, si mtoto aliyekwishawahi kuasiliwa kwa amri ya mahakama chini ya Sheria hii, itathibitishwa kiasi cha kuiridhisha mahakama kuwa utambulisho wa mtoto huyo unafanana na mtoto ambaye taarifa zake zipo kwenye Rejesta ya vizazi, amri yoyote ya kuasili itokanayo na maombi itajumuisha maelekezo kwa Msajili Mkuu kuingiza taarifa katika Rejesta ya vizazi kwa kuweka maneno “Aameasiliwa”

(5) Endapo amri ya kuasili itatolewa na mahakama chini ya Sheria hii, amri hiyo itajumuisha maelekezo kwa Msajili Mkuu kuagiza kuingizwa kwa taarifa za awali katika Rejesta ya watoto walioasiliwa kuweka maneno “Ameasiliwa”.

(6) Endapo amri ya kuasili itatolewa na mahakama chini ya Sheria hii, mahakama itaagiza kupelekwa amri hiyo kwa Msajili Mkuu kwa namna ilivyoainishwa na baada ya kupokea taarifa hiyo, Msajili Mkuu ataagiza kutekelezwa kwa amri hiyo kuhusiana na kuingiza taarifa katika Rejesta ya vizazi kwa neno “Ameasiliwa” na kuingizwa taarifa husika katika Rejesta ya watoto walioasiliwa.

Marekebisho  
ya amri na  
masahihisho  
ya Rejesta

71.-(1) Mahakama iliyotoa amri ya kuasili chini ya Sheria hii yaweza, kwa maombi ya mzazi aliyeasili au mtoto aliyeasiliwa, kurekebisha amri kwa kufanya masahihisho ya kosa lolote mahususi, na pale ambapo amri ya kuasili imerekeblishwa, Mahakama itawezesha marekebisho hayo kuwasili kwa Msajili Mkuu kama ilivyoainishwa.

(2) Uwezo wa mahakama chini ya kifungu kidogo cha (1) utajumuisha uwezo wa kurekebisha amri -

- (a) kwa kuingiza nchi ambayo mtoto aliyeasiliwa amezaliwa; au
- (b) iwapo hajjaainisha tarehe halisi aliyozaliwa mtoto aliyeasiliwa, kwa kuingiza tarehe ambayo Mahakama itaona kuwa ndiyo tarehe inayowezekana kuwa mtoto alizaliwa, na masharti ya kifungu kidogo cha (1) yatatumika kama yalivyo.

(3) Endapo rufaa dhidi ya amri ya kuasili itakubaliwa, mahakama iliyotoa amri itatoa maelekezo kwa Msajili Mkuu kuondoa alama zozote katika taarifa zozote kwenye Rejesta ya vizazi na taarifa zozote kwenye Rejesta ya watoto walioasiliwa ambazo ziliingizwa

kutokana na amri hiyo.

Kukatazwa  
kwa malipo  
na zawadi  
katika kuasili

72.-(1) Mtu hatatoa malipo au zawadi yoyote kwa ajili ya amri ya kuasili isipokuwa kwa amri ya mahakama.

(2) Mtu hatapokea malipo au zawadi yoyote kwa ajili ya mpango wowote ambao unaweza kupelekea au kusababisha kutolewa kwa amri ya kuasili.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Notisi  
kutolewa ili  
kupeleka  
mtoto nje

73.-(1) Mzazi aliyeasili atamuarifu Kamishna kwa maandishi wakati mtoto aliyeasiliwa anapelekwa nje ya nchi kwa kipindi cha kudumu baada ya amri ya kuasili kutolewa na Mahakama.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), notisi itawasilishwa kwa Kamishna ndani ya siku thelathini kabla ya mzazi aliyeasili na mtoto aliyeasiliwa kuondoka nchini.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi na isiyozidi milioni hamsini au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Uasili kwa  
wageni

74.-(1) Mtu asiye raia wa Tanzania anaweza kumwasili Mtanzania iwapo-

- (a) mtoto hawesi kuwekwa kwenye malezi ya kambo au familia ilioasili au hatoweza kutunzwa kwa namna yenyе maslahi kwa mtoto wakati akiwa Tanzania;
- (b) ameishi Tanzania kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo;
- (c) amemlea mtoto kama mlezi wa kambo kwa kipindi cha angalau miezi mitatu chini ya usimamizi wa Afisa Ustawi wa Jamii;
- (d) hana kumbukumbu yoyote ya makosa ya jinai nchini kwake au kwenye nchi nyingine yoyote;
- (e) ana mapendekezo kutoka kwa Afisa Ustawi wa Jamii kutoka nchini mwake na mamlaka nyingine husika kutoka nchi yake

- ya makazi ya kudumu yanayoonyesha kuwa anastahili kuasili mtoto;
- (f) ameiridhisha mahakama kuwa nchi yake ya asili inaheshimu na kutambua amri ya kuasili.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), Mahakama yaweza kutoa amri ya kuasili endapo ni kwa maslahi ya mtoto.

(3) Kwa maombi ya kuasili kutoka kwa mgeni Afisa Ustawi wa Jamii atapaswa kufanya uchunguzi kwa mwombaji na kuwasilisha taarifa ya uchunguzi wa kijamii mahakamani ili kuisaidia mahakama kutoa maamuzi.

(4) Mahakama yaweza, kwa maombi ya kuasili yanayofanywa na mgeni, kutoa amri ya ziada -

- (a) kumtaka Afisa Ustawi wa Jamii kusimamia maslahi ya mtoto;
- (b) kumtaka Afisa Ustawi wa Jamii kuandaa taarifa ya uchunguzi wa kijamii kuisaidia mahakama kuamua iwapo amri ya kuasili ni kwa maslahi ya mtoto au la; au
- (c) kuhusu jambo jingine lolote kama mahakama itakavyoamua.

Kanuni za  
kuasili

75.-(1) Waziri mwenye dhamana na ustawi wa jamii kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana na masuala ya watoto anaweza, kutengeneza kanuni zitakazoainisha utaratibu wa kuendesha mashauri ya kuasili.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) kanuni hizo zitaainisha-

- (a) mashauri yatakayoendeshwa kwa faragha isipokuwa katika mazingira ya kipekee;
- (b) kukubalika kwa ushahidi wa kimaandishi unaohusiana na idhini inayohitajika katika amri;
- (c) hitaji la Afisa Ustawi wa Jamii kusimamia maslahi ya mtoto;
- (d) sharti la Afisa Ustawi wa Jamii kuandaa taarifa ya uchunguzi wa kijamii ya kuisaidia mahakama kuamua iwapo amri ya kuasili ni kwa maslahi ya mtoto au la; na
- (e) jambo jingine lolote ambalo Waziri wa ustawi wa jamii ataamua.

Masharti

76.-(1) Itakuwa ni kosa kuchapisha tangazo lolote lenye maelezo

katika uchapishaji na matangazo yanayoonyesha kwamba-

- (a) Mzazi au mlezi wa mtoto anataka au anaagiza kuwa mtoto aasiliwe;
- (b) mtu anataka kuasili mtoto; au
- (c) mtu yuko tayari kufanya mipango kwa ajili ya mtoto kuasiliwa.

(2) Mtu yejote ambaye atasababisha kuchapishwa au akiwa anafahamu anachapisha tangazo linalokiuka masharti ya kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria hii na atakapotiwa hatiani atalipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

**SEHEMU YA SABA**

**AJIRA YA MTOTO**

*(a) Ajira ya mtoto*

Haki ya mtoto kufanya kazi 77.-(1) Mtoto atakuwa na haki ya kufanya kazi nyepesi.

(2) Kwa madhumini ya kifungu kidogo cha (1), umri wa chini wa mtoto kuajiriwa utakuwa ni miaka kumi na nne.

(3) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), kazi nyepesi itajumuisha kazi ambazo hazina madhara kwa afya na maendeleo ya mtoto na hazitamzuia mtoto au kuathiri maudhurio ya mtoto shulen, kushiriki katika programu za mafunzo ya ufundi au uwezo wa mtoto kufaidika na kazi za shulen.

Kukatazwa kwa kazi za kinyonyaji 78.-(1) Mtu hatamwajiri mtoto au kumshughulisha katika kazi yoyote ya kinyonyaji.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu hiki, kila mwajiri atahakikisha kuwa kila mtoto aliyeajiriwa au kushughulishwa kulingana na Sheria hii analindwa dhidi ya ubaguzi au vitendo vinavyoweza kuwa na madhara kwa mtoto kwa kuzingatia umri wake na uwezo wake wa kushiriki.

(3) Kazi itachukuliwa kuwa ya kinyonyaji iwapo -

- (a) inadhuru afya ya mtoto au kuathiri maendeleo yake;
- (b) inazidi saa sita kwa siku;
- (c) hailingani na umri wake; au
- (d) mtoto anapata malipo pungufu.

(4) Mtu yejote atakayekiuka masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atalipa faini isiyopungua shilingi laki moja au kifungo cha miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

Kukatazwa  
kwa kazi za  
usiku

79.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 78, mtoto hataajiriwa au kushughulishwa katika mkataba wa huduma ambao utamtaka mtoto kufanya kazi usiku.

(2) “Kazi za usiku” itatafsiriwa kujumuisha utendaji wa kazi ambao utamtaka mtoto kuwa kazini kati ya saa mbili usiku na saa kumi na mbili asubuhi.

(3) Mtu yejote atakayekiuka masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na, atakapotiwa hatiani atalipa faini isiyopungua shilingi laki moja au kifungo cha miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

Kukatazwa  
kwa kazi za  
kulazimi-  
shwa

80.-(1) Mtu yejote atakayeshawishi, atakayemtuma, atakayemtaka au atakayemlazimisha mtoto kufanya kazi atakuwa ametenda kosa.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, “kazi za kulazimisha” zitajumuisha kazi za kulazimisha au aina nyingine yoyote ya kazi anayopewa mtu kwa vitisho vya kupewa adhabu lakini hazitajumuisha kazi za kawaida za kiraia, huduma ndogo ndogo za kijamii zinazofanywa na wanajamii zenye maslahi ya moja kwa moja kwa jamii hiyo.

(3) Mtu yejote atakayekiuka masharti ya kifungu chochote cha kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua shilingi laki mbili au kifungo cha miezi sita au vyote kwa pamoja.

Haki ya ujira

81.-(1) Mtoto ana haki ya kulipwa ujira kulingana na thamani ya kazi aliyofanya.

Sura ya 366

(2) Bila kujali masharti ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, mwajiri yejote atakayekiuka kifungu hiki atakuwa ametenda kosa.

Ajira  
hatarishi

82.-(1) Itakuwa ni kinyume cha sheria kumwajiri au kumshughulisha mtoto katika kazi yoyote ambayo ni hatarishi.

(2) Kazi itatafsiriwa au itachukuliwa kuwa hatarishi iwapo inahatarisha afya, usalama au maadili ya mtu.

(3) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (3), kazi hatarishi zitajumuisha -

- (a) kazi za ubaharia;
- (b) uchimbaji madini au upasuaji mawe;
- (c) ubebaji wa mizigo mizito;
- (d) viwanda vyta uzalishaji ambamo kemikali zinazalishwa au kutumika;
- (e) kufanya kazi katika sehemu ambazo mashine zinatumika; na
- (f) kufanya kazi katika sehemu kama vile baa, hoteli na sehemu za starehe.

(4) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (3) sheria yoyote inayosimamia utoaji wa mafunzo yaweza kuruhusu mtoto -

- (a) kufanya kazi katika meli ya mafunzo kama sehemu ya mafunzo ya mtoto;
- (b) kiwandani au machimboni, endapo kazi hiyo ni sehemu ya mafunzo kwa mtoto huyo;
- (c) katika sehemu nyingine yoyote ya kazi kwa masharti kwamba afya, usalama na maadili ya mtoto yanalindwa kikamilifu na kuwa mtoto anapokea au kupata maelekezo maalum na ya kutosha katika mafunzo au yanayo endana na shughuli husika.

Kukatazwa  
kwa  
unyanyasaji  
wa  
kimapenzi

83.-(1) Mtoto hataajiriwa katika kazi au biashara yoyote itakayompelekea kujihusisha na masuala ya kimapenzi kwa malipo au la.

(2) Kwa kuondoa shaka itakuwa ni kinyume cha sheria kwa mtu yeyote kutumia-

- (a) vishawishi au shuruti kumshawishi mtoto kujihusisha na masuala ya kimapenzi;
- (b) watoto katika shughuli za ukahaba au vitendo vyovyyote vyta kimapenzi; na
- (c) watoto katika picha za maonyesho ya ngono au vitu vinavyohusika na hivyo.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka kifungu hiki atakuwa ametenda kosa na atakapotiya hatiani atalipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kusichopungua mwaka mmoja na kisichozi miaka ishirini au vyote kwa pamoja.

Matumizi

84.-(1) Kwa kuondoa mashaka, Sehemu hii itatumika katika ajira

ya sekta rasmi na isiyo rasmi.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), afisa kazi, katika muda wowote muafaka, ataingia katika eneo lolote na kufanya ukaguzi ambaon ni lazima ili kujiridhisha kwamba masharti ya Sehemu hii yanatekelezwa.

(3) Kwa madhumuni ya sehemu hii, neno “eneo” litakuwa na maana ya jengo, ofisi, kiwanja, shamba, mahali, saiti na litajumuisha chombo cha usafiri majini, chombo cha moto na ndege.

Usajili wa mtoto katika shughuli za viwandani

85.-(1) Mwajiri katika kiwanda chochote atakuwa na rejesta ya watoto aliowaajiri au kuwashughulisha na tarehe zao za kuzaliwa iwapo zinafahamika au umri unaokisiwa iwapo tarehe zao za kuzaliwa hazifahamiki.

(2) Shughuli za viwandani ni shughuli zote za viwanda isipokuwa za kibashara au kilimo na zitajumuisha -

- (a) migodi, machimbo ya mawe na shughuli nyingine za uchimbaji wa madini toka ardhini;
- (b) shughuli ambazo vitu vinatengenezwa, vinabadilishwa, vinasafishwa, vinakarabatiwa, vinanakshiwa, yanakamilishwa, vinabadilishwa kwa ajili ya kuuzwa, vinavunjwa au kuharibiwa, au ambamo vitu vinabadilishwa ikijumuisha shughuli za ujenzi wa meli au katika kuzalisha, kubadilisha au kusafirisha umeme au nguvu za aina yoyote; na
- (c) shughuli za kusafirisha abiria au mizigo kwa barabara au reli ikijumuisha ubebaji wa mizigo bandarini, kwenye gati, vivuko ghala au viwanja vya ndege.

Utekelezaji

86.-(1) Afisa kazi atafanya udadisi anaoona ni wa lazima ili kujiridhisha kwamba masharti ya vifungu vya Sehemu hii vinavyohusiana na ajira ya watoto yanafuatwa kwa umakini.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, afisa kazi anaweza kumhoji mtu ye yeyote kama italazimika.

(3) Endapo afisa kazi atajiridhisha kwamba masharti ya sehemu hii yamekiukwa, atatoa amri ya kutokufuata sheria kwenye ajira na atatoa taarifa kwa Afisa Ustawi wa Jamii na kwenye kituo cha polisi cha karibu ambaon watapeleleza na kuchukua hatua stahili ili kumlinda mtoto.

*(b) Mafunzo ya ufundi*

- |  |   |
|--|---|
| Haki ya<br>kupata<br>weledi katika<br>ufundi | 87. Mtoto atakuwa na haki ya kupata weledi katika nyanja za<br>ufundi na mafunzo ya ufundi.   |
| Umri wa<br>chini kwa<br>mafunzo ya<br>ufundi | 88. Umri wa chini kwa mtoto kuanza mafunzo ya ufundi na fundi<br>mchundo utakuwa miaka kumi na nne au mara baada ya kumaliza<br>elimu ya msingi   |
| Jukumu la<br>fundi<br>mchundo                | 89. Majukumu ya fundi mchundo kwa mwanagenzi aliye chini<br>yake litakuwa-<br><ul style="list-style-type: none"><li>(a) kumfundisha na kumwelekeza mwanagenzi kwenye<br/>shughuli kwa kadri ya uwezo, utaalamu na ujuzi alionao<br/>na kwa kadri ya uwezo wa mwanagenzi huyo au<br/>kumfanya mwanagenzi ajifunze kwenye shughuli chini<br/>ya usimamizi wake;</li><li>(b) kuwajibika na madhara yoyote atakayopata mwanagenzi<br/>wakati wa mafunzo;</li><li>(c) kumpatia mwanagenzi mazingira safi na salama;</li><li>(d) kumwandaa mwanagenzi kuwa na ari ya kuendesha<br/>maisha ya kujitegemea; na</li><li>(e) kulinda maslahi ya mwanagenzi kwa ujumla.</li></ul>  |
| Makubaliano<br>ya mafunzo<br>ya ufundi       | 90.-(1) Mzazi, mlezi au ndugu wa mwanagenzi atafanya<br>makubaliano ya mafunzo ya ufundi na fundi mchundo.<br><br>(2) Makubaliano yatafanywa kulingana na desturi zinazohusiana<br>na shughuli husika lakini hazitajumusha sherehe yoyote ambayo<br>inakinzana na haki za mtoto zilizoainishwa kwenye Sheria hii.<br><br>(3) Makubaliano yatakuwa na mambo yaliyokubaliwa na pande<br>zote mbili na yatajumuisha -<br><ul style="list-style-type: none"><li>(a) sharti kifungu kuwa mzazi, mlezi, ndugu au fundi mchundo<br/>atabeba gharama za mavazi ya kumlinda na vifaa vyta<br/>msingi kwa mafunzo ya mwanagenzi;</li><li>(b) wajibu wa fundi mchundo ni kumpatia mwanagenzi sehemu<br/>ya malazi; na</li><li>(c) sharti kuwa fundi mchundo atampatia mwanagenzi posho</li></ul> |

isiyopungua nusu ya kima cha chini cha mshahara kwa siku kwa ajili ya kujikimu, endapo mwanagenzi anazalisha kipato.

(4) Makubaliano yatakuwa kwa maandishi na yatajumuisha masharti yatakayoonyesha maslahi ya pande zote mbili na mwanagenzi.

(5) Endapo upande wowote utakiuka masharti, mkataba utavunjika papo hapo isipokuwa kama kuna nia tofauti katika mkataba.

Wajibu wa  
Mwanagenzi

91. Mwanagenzi atamtii fundi mchundo kwa umakini na uaminifu na atamtumikia fundi mchundo na atakubali -

- (a) kuhudhuria mafunzo ya ufundi mara mara;
- (b) kuzuia uharibifu wa makusudi wa mali za fundi mchundo; na
- (c) kutokuficha uharibifu wowote utakaotokea kwenye mali za ufundi mchundo.

Kuruhusiwa  
kwa  
mwanagenzi

92.-(1) Masharti ya kuruhusiwa kwa wanagenzi baada ya kukamilisha mafunzo yake, hayatakuwa ya kinyonyaji na yatakuwa kulingana na maslahi ya mtoto.

(2) Fundi mchundo, baada ya kukamilika kwa mafunzo ya ufundi, atampatia mwanagenzi uthibitisho wa kumruhusu kutoka katika mafunzo ya ufundi.

Usuluhishi  
wa mgogoro

93. Mgogoro wowote utakaotokana na makubaliano ya mafunzo ya ufundi utapelekwa na watusika kwa Afisa Kazi wa Wilaya husika wa makubaliano wa mafunzo ya ufundi.

**SEHEMU YA NANE**  
**HUDUMA ZA KUMSAIDIA MTOTO TOKA KWENYE**  
**MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA**

Wajibu wa  
Serikali za

94.-(1) Serikali ya mtaa itakuwa na wajibu wa kulinda na kukuza ustawi wa mtoto ndani ya eneo lake.

Mtaa kulinda

watoto na  
kukuza  
uhusiano  
baina ya  
wazazi na  
watoto

(2) Afisa Ustawi wa Jamii katika Serikali za Mitaa atatekeleza majukumu yake yanayohusiana na ustawi wa watoto, na anaweza kusaidiwa na maofisa wa Serikali za mitaa kwa namna mamlaka itakavyoamua.

(3) Mamlaka ya Serikali ya mtaa, kupitia Afisa Ustawi wa Jamii itatoa ushauri nasaha kwa wazazi wote, walezi, ndugu na watoto kwa madhumuni ya kukuza uhusiano baina yao.

(4) Mamlaka ya Serikali za Mitaa itakuwa na jukumu la kutunza Rejesta ya watoto walio katika mazingira hatarishi katika eneo lake na kutoa msaada kwao kila itakapowezekana ili kuwawezesha watoto hao kukuwa katika hali ya kiutu baina yao na watoto wengine na kuendeleza vipaji vyao na uwezo wa kujitegemea.

(5) Kila mamlaka ya serikali ya mtaa, katika eneo lake, itatakiwa kutoa msaada na makazi kwa mtoto ye yeyote ambaye mamlaka itaona anahitaji msaada huo kutokana na kupotea au kutelekezwa au akiwa anahitaji hifadhi.

(6) Kila mamlaka ya serikali ya mtaa, kwa kushirikiana na polisi itafanya kila jithada kuwatafuta wazazi, walezi au ndugu wa mtoto aliyepotea au aliyetelekezwa na, kumrudisha mtoto huyo mahali alipokuwa akiishi, na iwapo mamlaka itashindwa kufanya hivyo, italipeleka suala hilo kwa Afisa Ustawi wa Jamii.

(7) Afisa Ustawi wa Jamii na askari wa polisi katika mamlaka ya serikali ya mtaa, watapeleleza mashauri yote ya uvunjaji ama ukiukwaji wa haki za mtoto.

Wajibu wa  
kuripoti  
ukiukwaji wa  
haki za mtoto

95.-(1) Utakuwa ni wajibu wa kila mwanajamii ambaye ana ushahidi au taarifa kwamba haki za mtoto zinakiukwa au mzazi, mlezi na ndugu anayemlea mtoto ana uwezo, lakini hataki kumpatia mtoto chakula, malazi, haki ya kucheza na kufurahi, mavazi, huduma za afya na elimu au kumtelekeza, kuripoti suala hilo kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa ya eneo hilo.

(2) Afisa Ustawi wa Jamii anaweza, baada ya kupokea taarifa, kumwitwa mtu aliyetolewa taarifa kujadili suala hilo; na maamuzi yatatolewa na afisa huyo kwa kuzingatia maslahi ya mtoto.

(3) Endapo mtu ambaye taarifa imetolewa dhidi yake atakataa kutekeleza maamuzi yaliyofanywa katika kifungu kidogo cha (2), Afisa Ustawi wa Jamii atalipeleka suala hilo mbele ya mahakama ambayo italisikiliza shauri hilo na kulitolea maamuzi, na katika shauri hilo mahakama yaweza -

- (a) kutoa nafuu yoyote au kutoa amri iliyokuwa imeombwa kwa jinsi mazingira yatakavyo ruhusu; na
- (b) kwa upande wa mzazi, pamoja na nafuu au amri itamwamuru mzazi kuweka dhamana ya kutoa malezi na uangalizi kwa kutia saini na kuahidi kumpatia mtoto mahitaji yote muhimu.

(4) Kwa masharti ya Sheria hii, mahakama ya mwanzo inaweza kuwa ndiyo mahakama ya nganzi ya kwanza kusikiliza mashauri katika sehemu hii na rufaa kutoka mahakama hiyo zitafuata taratibu za kawaida za rufaa.

(5) Mtu yejote atakayekiuka kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa, na atakapotiwa hatiani atalipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini au kifungo kwa kipindi cha miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

Upelezei  
utakaofa-  
nywa na  
Idara

96.-(1) Endapo Afisa Ustawi wa Jamii atakuwa na sababu za msingi kushuku kuwepo kwa unyanyasaji wa mtoto au kuhitajika kwa malezi na ulinzi wa mtoto, akiambatana na askari polisi, anaweza kuingia na kufanya upekuzi katika eneo lolote ambalo mtoto amewekwa kwa lengo la kufanya uchunguzi.

(2) Endapo baada ya uchunguzi itathibitika kwamba mtoto amekuwa akinyanyaswa au kuhitaji malezi na ulinzi wa haraka, Afisa Ustawi wa Jamii, akiambatana na askari wa polisi, watamwondoa mtoto na kumweka katika shehemu yenye usalama kwa kipindi kisichozidi siku saba.

(3) Endapo mtoto atakuwa amehamishwa au kuondolewa kulingana na kifungu kidogo cha (2), Afisa Ustawi wa Jamii atampeleka mtoto huyo mbele ya mahakama ndani ya siku kumi na nne ili amri itolewe.

(4) Mahakama yaweza kumweka mtoto kwenye nyumba ya makao yaliyothibitishwa au chini ya ulezi wa Afisa Ustawi wa Jamii au mtu mwingine yejote anayefaa hadi hapo mahakama

itakapomaliza kulisikiliza shauri hilo.

**SEHEMU YA TISA**  
**MTOTO ANAYEKINZANA NA SHERIA**  
*(a) Mahakama ya Watoto*

Kuanzishwa  
kwa  
Mahakama  
ya Watoto

97.-(1) Kutaanzisha mahakama itakayojulikana kama Mahakama ya Watoto, kwa madhumuni ya kusikiliza na kuamua masuala yanayohusiana na watoto.

(2) Jaji Mkuu aweza, kwa notisi itakayochapishwa kwenye *Gazeti la Serikali*, kuteua jengo lolote linalotumiwa kama mahakama ya mwanzo kuwa Mahakama ya Watoto.

(3) Hakimu Mkazi atapewa jukumu la kusikiliza mashauri katika Mahakama ya Watoto.

Mamlaka ya  
Mahakama  
ya Watoto

98.-(1) Mahakama ya Watoto itakuwa na mamlaka ya kusikiliza na kuamua-

- (a) mashtaka ya jinai dhidi ya mtoto; na
- (b) maombi yanayohusiana na malezi, matunzo na ulinzi wa mtoto.

(2) Mahakama ya Watoto itakuwa pia na mamlaka na uwezo utakaotolewa kwake na sheria nyingine yoyote.

(3) Mahakama ya Watoto, pale itakapowezekana, itakaa katika jengo tofauti na jengo ambalo kwa kawaida hutumika kusikiliza kesi za watu wazima.

Utaratibu  
katika  
Mahakama  
ya Watoto

99.-(1) Utaratibu wa kuendesha mashauri katika Mahakama ya Watoto katika masuala yote utakuwa ni kulingana na kanuni zitakazotungwa na Jaji Mkuu kwa madhumuni hayo, lakini kwa namna yoyote zitakuwa ni kulingana na masharti yafuatayo-

- (a) Mahakama ya Watoto itakaa mara nyingi kama itakavyo lazimu;
- (b) mashauri yataendeshwa kwa faragha;
- (c) kwa kadri itakavyowezekana mashauri yataendeshwa kwa njia isiyo rasmi, na yataendeshwa kwa kuuliza maswali bila kumweka mtoto katika taratibu za kiadvesari;
- (d) Afisa Ustawi wa Jamii atahudhuria;
- (e) mzazi, mlezi au mtu anayemwakilisha mtoto watakuwa na haki

- ya kuhudhuria;
- (f) mtoto atakuwa na haki ya kuwa na ndugu wa karibu na kuwakilishwa na wakili;
  - (g) haki ya kukata rufaa itawekwa bayana kwa mtoto; na
  - (h) mtoto atakuwa na haki ya kujieleza na kutoa maoni.

(2) Mbali ya wajumbe na maafisa wa Mahakama ya Watoto, watu wafuatao tu, kwa ridhaa ya mahakama, wanaweza kuhudhuria kikao chochote cha Mahakama ya Watoto-

- (a) wahusika wa kesi iliyoko mbele ya mahakama, mawakili wao, mashahidi na watu wengine ambao wamehusika moja kwa moja au wameshiriki katika kesi; na
- (b) mtu mwingine yejote ambaye mahakama itamruhusu kuwepo

Mashauri  
katika  
Mahakama  
za Watoto

100.-(1) Mahakama ya Watoto inaposikiliza kesi dhidi ya mtoto, kama inawezekana, isipokuwa kama mtoto ameshtakiwa pamoja na mtu mwingine ambaye si mtoto, itakaa katika jengo au chumba tofauti na kile ambacho hutumika kuendesha mashauri ya kawaida ya mahakama.

Sura za 11 na  
20

(2) Endapo wakati wa kusikiliza shauri lolote mahakamani, mahakama itaona kuwa mtu aliyeshitakiwa au mtu ambaye shauri hilo linamhusu ni mtoto, mahakama itaahirisha kusikiliza shauri na kumpeleka mtoto kwenye mahakama ya watoto.

Dhamana  
kwa mtoto

(3) Endapo wakati wa kusikiliza mashauri yoyote katika Mahakama ya Watoto itaonekana kuwa mtu aliyeshitakiwa au mtu ambaye shauri hilo linamhusu ni mtu mzima, mahakama itaendelea kusikiliza na kuamua shauri hilo kulingana na masharti ya Sheria ya Mahakimu wa Mahakama au Sheria ya Mwenendo wa Jinai, kama hali itakavyokuwa.

101. Endapo mtoto ameshikiliwa kwa hati ya kukamata au la, na kama hawesi kupelekwa mbele ya Mahakama ya Watoto mara moja, afisa mfwidhi wa kituo cha polisi ambacho mtoto amepelekwa-

- (a) isipokuwa kama shitaka ni la mauaji au kosa lolote ambalo adhabu yake ni kifungo kinachozidi miaka saba;
- (b) isipokuwa kama itakuwa ni lazima kwa maslahi ya mtoto kumwondoaa asikae pamoja na mtu asiyefaa; au
- (c) isipokuwa kama afisa huyo ana sababu za kuamini kuwa kuachiliwa kwa mtoto huyo kutaathiri utoaji haki,

anaweza kumwachilia mtoto huyo kwa kujidhamini mwenyewe au

kwa kudhaminiwa na mzazi, mlezi au ndugu au bila kuwa na wadhamini.

Kukaa  
pamoja na  
watu wazima  
akiwa  
mahabusi

Mahakama  
ya Watoto  
yaweza  
kusikiliza  
kesi zote  
isipokuwa za  
mauaji

Watoto  
wanaweza  
kuwekwa  
chini ya  
uangalizi wa  
mtu anayefaa  
au taasisi

Wajibu wa  
mahakama  
wa kuelezea  
shitaka

Mshtakiwa  
kutakiwa  
kutoa sababu

Mshitakiwa  
anaweza  
kutiwa  
hatiani kwa  
kukubali  
kosa

Kuhudhuria  
na

102. Askari wa polisi ataandaa utaratibu wa kumtenga mtoto kwa namna itakavyowezekana, wakati akiwa mahabusi ili asikae pamoja na mtu mzima aliyeshitakiwa kwa kosa la jamii naye isipokuwa kama ni ndugu yake.

103.-(1) Afisa wa polisi hatampeleka mtoto mahakamani isipokuwa kama upelelezi umekamilika au kama kosa linahitaji kusikilizwa ili kupata uamuji wa kupelekwa Mahakama Kuu.

(2) Endapo mtoto amepelekwa mbele ya Mahakama ya Watoto kwa kosa lolote isipokuwa la mauaji, kesi hiyo itasikilizwa na kuamuliwa siku hiyo hiyo.

104.-(1) Endapo Mahakama ya Watoto inamweka mtoto mahabusi, au inaanua kuwa apelekwe katika Mahakama Kuu na mtoto hajaachiliwa kwa dhamana au hajaachiliwa huru, Mahakama ya Watoto yaweza, badala ya kumweka mtoto mahabusi, kutoa amri awekwe chini ya uangalizi wa Kamishna, mtu anayefaa au taasisi iliyotajwa kwenye amri.

(2) Mtoto atabaki chini ya uangalizi wa mtu huyo au taasisi kwa kipindi kilichotajwa kwenye amri au mpaka atakaposhughulikiwa kulingana na sheria na itachukuliwa kwamba yupo kwenye ulinzi kisheria mpaka wakati huo.

105. Wakati Mahakama ya Watoto itakapokuwa inasikiliza shitaka dhidi ya mtoto itawajibika kutoa maeleo ya kosa husika katika lugha nyepesi.

106. Baada ya kumwelezea maeleo ya kosa, Mahakama ya Watoto itamtaka mtoto atoe tamko endapo ana sababu itakayomfanya asitiwe hatiani.

107. Pale ambapo tamko lililotolewa na mtoto linapelekea kukubali kosa, mahakama inaweza kumtia hatiani.

108.-(1) Endapo mtoto atakataa kosa aliloshtakiwa nalo, au

kusikilizwa kesi katika mahakama ya watoto iwapo mahakama itakataa tamko la mtoto kwamba limepelekea kukiri kosa kwa shitaka hilo, mahakama itaendelea kusikiliza ushahidi wa mashahidi wa upande wa mashtaka.

(2) Katika mashauri yote dhidi ya mtoto, iwapo wazazi, mlezi, ndugu au Afisa Ustawi wa Jamii anahudhuria, yejote kati yao anaweza, kwa ridhaa ya mahakama, kumsaidia mtoto aliyeshtakiwa kuendesha kesi yake, na haswa katika mahojiano na mashahidi wa upande wa mashtaka.

Kumhoji shahidi

109. Wakati wa kufunga ushahidi wa kila shahidi, Mahakama ya Watoto itawauliza mashahidi maswali ambayo itaona ni lazima au yanafaa, au kwa lengo la kupata ukweli wa shahidi au wa maelezo yaliyotolewa au kupima uadilifu wa shahidi.

Utetezi

110. Endapo baada ya mashahidi wa upande wa mashtaka kutoa ushahidi na mahakama imeridhika kwamba ushahidi uliotolewa mbele yake unaonyesha kuwa mtoto ana kesi ya kujibu, mahakama itawasikiliza mashahidi wa utetezi na maelezo yoyote ambayo mtoto atapenda kuyatoa katika utetezi wake.

Utaratibu baada ya kutiwa hatiani

111.-(1) Endapo mtoto atakiri kosa na mahakama ya watoto ikakubali kukiri huko au baada ya kusikiliza mashahidi Mahakama imeridhika kuwa kosa limethibitishwa, mahakama itamtia mtoto hatiani baada ya hapo, isipokuwa kama mazingira ni hafifu kiasi cha kutohitaji utaratibu huo kufuatwa, itapokea taarifa kuhusiana na mwenendo, mambo ya nyuma, maisha ya nyumbani, kazini na afya ya mtoto ili kuiwezesha mahakama kulishughulikia suala hilo kwa maslahi ya mtoto, na inaweza kumuuliza swali lolote lililotokana na taarifa hizo.

(2) Kwa madhumuni ya kupata taarifa au uchunguzi maalum wa kitabibu au mtazamo Mahakama ya Watoto inaweza kumweka mtoto mahabusi au kumwachilia kwa dhamana.

Wazazi wa mtoto aliyeshtaki-wa kuhudhuria mahakamani

112. Endapo mtoto ameshtakiwa na kosa lolote, mahakama yenyewe inaweza kumtaka mzazi wake, mlezi, ndugu au Afisa Ustawi wa Jamii kuhudhuria mahakamani na inaweza kutoa amri yoyote kama itakavyoona inafaa ili kuhakikisha wanahudhuria.

Uamuzi kuhusu umri

113.-(1) Endapo mtu, ameshtakiwa kwa kosa au la, analetwa mbele ya Mahakama yoyote kwa sababu yoyote mbali na kutoa

ushahidi na mahakama ikaona kuwa ni mtoto, mahakama itafanya udadisi kuhusu umri wa mtu huyo.

(2) Mahakama itachukua ushahidi katika kusikiliza kesi hiyo ambao unaweza kujumuisha ushahidi wa kitabibu au, na kipimo cha Vinasaba vya Binadamu kama itakuwa ni lazima ili kupata uthibitisho wa kuzaliwa, au wa maandishi au vinginevyo kwa namna mahakama itakavyoona itaamini.

(3) Cheti kinachosadikiwa kuwa kimesainiwa na mtatibu aliyesajiliwa au mwenye leseni chini ya Sheria inayosimamia masuala ya tiba Tanzania kuhusiana na umri wa mtoto kitakuwa ni ushahidi wa kutosha na kinaweza kupokelewa na mahakama bila uthibitisho wa saini isipokuwa kama mahakama itaamuru vinginevyo.

(4) Amri au hukumu ya mahakama haitabatilishwa kwa ushahidi wowote utakaletwa baadaye kwamba umri wa mtu huyo haukuwa sahihi kama ulivyonajwa mahakamani na umri utakaokuwa umeamuliwa na mahakama kuwa ni umri wa mtu aliyeletwa mahakamani, kwa madhumuni ya kifungu hiki, utakuwa ndiyo umri sahihi wa mtu huyo.

(5) Ushahidi wa kitabibu na, au kutolewa damu kwa lengo la kufanya kipimo cha Vinasaba vya Binadamu utafanyika mbele ya Afisa Ustawi wa Jamii.

Watu  
wanaoone-  
kana kuwa na  
umri wa  
miaka kumi  
na nane au  
zaidi

114.-(1) Endapo mahakama itaona kwamba mtu aliyeletwa mbele yake ana umri zaidi ya miaka kumi na nane, kwa madhumuni ya kifungu hiki, mtu huyo atakuwa si mtoto.

(2) Bila kuathiri masharti yaliyopita ya kifungu hiki, iwapo mahakama itashindwa kuthibitisha umri sahihi wa mtu aliyeletwa mbele yake, basi umri uliotajwa na mtu huyo, mzazi, mlezi ndugu au

Afisa Ustawi wa Jamii utachukuliwa kuwa ndio umri sahihi wa mtu huyo.

*(b) Mtoto shahidi*

Shahidi  
Mtoto

115.-(1) Endapo kwenye shauri au suala lolote mtoto aliyeitwa kama shahidi, kwa maoni ya mahakama, haelewii maana ya kiapo,

ushahidi waweza kuchukuliwa, kama kwa maoni ya mahakama, maoni ambayo yatarekodiwa kwenye mwenendo wa kesi, mtoto ana uelewa wa kutosha wa sheria ya ushahidi na anaelewa, wajibu wa kusema ukweli.

(2) Bila kujali kanuni zozote za sheria au utaratibu tofauti, iwapo ushahidi uliopokelewa kupitia kifungu kidogo cha (1) ultolewa kwa upande wa mashtaka na haukutiliwa nguvu na ushahidi mwininge wowote wa msingi unamkandamiza mshitakiwa, mahakama inaweza, baada ya kuchukua tahadhari, kutumia ushahidi huo kumtia hatiani mshitakiwa kama itaridhika kikamilifu kwamba mtoto anasema ukweli.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu hiki, iwapo kwenye shauri lolote linalohusisha kosa la kujamiiiana ushahidi wa pekee ni ule wa mtoto au wa mwathirika wa kosa la kujamiiiana, mahakama itaupokea ushahidi huo na baada ya kutathmini uaminifu wa mtoto au mwathirika wa kosa la kujamiiiana kwa maoni yake bila ya kujali kwamba ushahidi huo haujatiliwa nguvu, itamtia hatiani kwa sababu ambazo zitawekewa kumbukumbu katika mwenendo wa kesi, endapo mahakama itaridhika kuwa mtoto anasema ukweli tupu.

Sura ya 16

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki na sheria nyingine zozote, “kosa la kujamiiiana” linamaanisha kosa la kujamiiiana kama lilivyo ainishwa na Sheria ya Kanuni za Adhabu.

*(c) Hukumu ya kuwa chini ya uangalizi*

Amri ya  
kuwekwa  
chini ya  
uangalizi

116.-(1) Endapo mtoto atatiwa hatiani kwa kosa lolote ambalo si kosa la mauaji, Mahakama ya Watoto inaweza kutoa amri ya kumwachilia mkosaji kwa masharti baada ya kupata dhamana, ama kwa kudhaminiwa au la, ambaye atakuwa na tabia nzuri kwa kipindi hicho kisichozidi miaka mitatu, kama itakavyokuwa imeainishwa kwenye amri ila endapo mtoto ataonyesha tabia nzuri basi itachukuliwa kwamba mtoto huyo ametumikia adhabu hiyo.

(2) Dhamana itakavyokuwa imetolewa chini ya kifungu hiki, iwapo mahakama itaamuru hivyo, itajumuisha sharti kwamba mtoto awe chini ya uangalizi wa mzazi, mlezi, ndugu au Afisa Ustawi wa Jamii, kama itakavyokuwa imetajwa kwenye amri hiyo ndani ya kipindi kilichoainishwa katika amri, iwapo mtu huyo yuko tayari kutoa uangalizi pamoja na masharti mengine kwa ajili ya kupewa uangalizi kama yatakavyokuwa yameainishwa kwenye amri.

(3) Mtu aliyetajwa katika amri anaweza kuondolewa jukumu hilo wakati wowote, na katika hali hiyo au ikitokea mtu huyo aliyetajwa amefariki, mtu mwingine anaweza kuwekwa badala yake na Mahakama ya Watoto ambayo mtoto anabanwa na dhamana yake kuja mbele yake kutiwa hatiani au kuhukumiwa.

Masharti  
pale ambapo  
mtoto  
atashindwa  
kuzingatia  
masharti ya  
kuachiliwa

117.-(1) Endapo Mahakama ya Watoto imeridhika na taarifa iliyotolewa chini ya kiapo kwamba mtoto ameshindwa kuzingatia sharti lolote la dhamana, Mahakama itamuita mtoto huyo au kijana na wadhamini wake kama wapo, ikimuhitaji yeye au wao kuhudhuria katika Mahakama hiyo kwa wakati utakaoainishwa katika wito huo.

(2) Mahakama ya Watoto ambayo kwayo mtoto anabanwa na dhamana kuja mbele yake kwa hukumu, itakaporidhika kwamba ameshindwa kuzingatia masharti yoyote ya dhamana yake, inaweza kumshugulikia moja kwa moja kama vile inavyoweza kumshugulikia katika kosa la asili.

Mamlaka ya  
kumwamuru  
mzazi kulipa  
faini badala  
ya mtoto

118.-(1) Endapo mtoto atapatikana na hatia kwa kosa lolote ambalo adhabu yake inaweza kuwa faini, kulipa fidia au gharama, na mahakama ikawa na maoni kuwa itakuwa ni kwa maslahi ya mtoto kwa kuamuru kulipwa faini, fidia au gharama, ama pamoja na adhabu nyingine au la, mahakama yaweza kuamuru faini, fidia au gharama iliyotolewa ilipwe na mzazi, mlezi au ndugu wa mtoto badala ya mtoto, isipokuwa kama mahakama itaridhika kwamba mzazi, mlezi au ndugu wa mtoto hawezikupatikana au hakuchangia katika kutenda kosa kwa kutoekutoa malezi bora kwa mtoto.

(2) Amri chini ya kifungu hiki yaweza kutolewa dhidi ya mzazi mlezi au ndugu ambaye baada ya kutakiwa kuhudhuria, ameshindwa kufanya hivyo, isipokuwa hakuna amri itakayotolewa kabla ya kumpa mzazi, mlezi au ndugu wa mtoto haki ya kusikilizwa.

(3) Kiwango chochote kitakachopaswa kulipwa na mzazi, mlezi au ndugu kinaweza kupatikana kutoka kwake kwa kulazimishwa au kifungo kama vile amri hiyo imetolewa baada ya mzazi, mlezi au ndugu wa mtoto kutiwa hatiani.

(4) Mzazi au mlezi anaweza kukata rufaa dhidi ya amri iliotolewa chini ya kifungu hiki.

(d) *Adhabu mbadala*

Katazo la  
adhabu ya  
kuwekwa  
chini ya  
uangalizi na  
adhabu  
mbadala

119.-(1) Mtoto hatahukumiwa kutumikia kifungo.

(2) Endapo mtoto atatiwa hatiani kwa kosa lolote ambalo adhabu yake ni kifungo, mahakama inaweza, pamoja na amri yoyote mbadala ambayo inaweza kutolewa chini ya Sheria hii -

- (a) kumwachia mtoto bila kutoa amri yoyote;
- (b) kuamuru mtoto arudishwe kwa gharama ya Serikali kwenda nyumbani kwao au katika Wilaya yake ya asili kama itakuwa ndani ya Tanzania; au
- (c) kuamuru mtoto kukabidhiwa kwa uangalizi wa mtu anayefaa au taasisi itakayotajwa katika amri au mtu huyo au taasisi iko tayari kuchukua jukumu hilo.

Wakati  
ambao amri  
ya  
kupelekwa  
katika shule  
ya  
maadilisho  
inaweza  
kutolewa

120.-(1) Endapo mtoto ametiwa hatiani kwa kosa ambalo kama lingekuwa limefanywa na mtu mzima angeadhibiwa kwa adhabu ya kifungo, mahakama yawenza kuamuru mtoto huyo apelekwe katika shule ya iliyothibitishwa.

(2) Amri iliyotajwa kwenye kifungu cha (1) haitatolewa isipokuwa kama mlezi wa shule ya maadilisho ambayo mtoto anatakiwa kupelekwa ameitaarifu Mahakama ya Watoto kwamba ana nafasi ambayo inaweza kujazwa na mtu ambaye amri inataka kutolewa dhidi yake.

(3) Amri itakayotolewa chini ya kifungu hiki itajulikana kama amri ya shule ya maadilisho.

**SEHEMU YA KUMI  
SHULE ZILIZOTHIBITISHWA**

Shule za  
Maadilisho

121.-(1) Waziri mwenye dhamana na ustawi wa jamii, anaweza kwa amri, kuanzisha shule au kutamka shule yoyote au taasisi kuwa shule iliyothibitishwa maadilisho kwa madhumuni ya Sheria hii.

(2) Waziri mwenye dhamana na ustawi wa jamii anaweza kwa notisi katika *Gazeti* la Serikali, kumteua mtu yejote au chombo cha watu kuwa mlezi au meneja wa shule iliyothibitishwa.

Uteuzi wa  
Bodi ya  
wageni

122.-(1) Waziri mwenye dhamana na ustawi wa jamii kwa amri, ataanzisha Bodi ya Wageni kwa kila shule iliyothibitishwa, Bodi ambayo itajumuisha-

- (a) Mbunge wa eneo ambalo shule ya maadilisho ilipo;
- (b) mlezi;
- (c) Afisa Ustawi wa Jamii;
- (d) Afisa Elimu wa Wilaya;
- (e) Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ambapo shule ya maadilisho ilipo;
- (f) Afisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya; na
- (g) Afisa Magereza wa Mkoa.

(2) Wajumbe wa Bodi watakuwa madarakani kwa mujibu wa nyadhifa zao.

Mamlaka ya Bodi

123.-(1) Bodi au mjambe yejote wa bodi kwa kibali cha mwenyekiti anaweza -

- (a) kutembelea shule mara kwa mara;
- (b) itisha vitabu, karatasi na kumbukumbu zinazohusiana na usimamizi na nidhamu ya shule;
- (c) kuhoji wafanyakazi na wanafunzi ambao wanaishi hapo au kwa kibali;
- (d) kukagua na kupima ubora na kiwango cha chakula cha wanafunzi;
- (e) kuchunguza mienendo ya nidhamu;
- (f) kuthibitisha iwapo vifaa husika vinatolewa kwa ajili ya elimu, mafunzo, ustawi na michezo kwa wanafunzi;
- (g) kupeleleza malalamiko yoyote yaliyotolewa na mwanafunzi au mfanyakazi; au
- (h) kuwa na uwezo mwingine kama ambavyo itakavyoainishwa.

(2) Bodi inaweza, pale ambapo itaona inabidi au inahitajika, kutoa mapendeleko yoyote kuhusiana na uendeshaji wa shule ya maadilisho kwa Waziri mwenye dhamana na ustawi wa jamii.

Amri ya Shule iliyo-thibitishwa,

124.-(1) Amri ya Shule iliyo-thibitishwa, itaainisha-

- (a) shule ambayo mtoto au kijana anapaswa kupelekwa; na
- (b) mtu atakayekuwa na wajibu kumpeleka kwenye shule hiyo.

(2) Kila amri itakuwa na taarifa ambayo, kwa maoni ya mahakama, ni muhimu kufahamika kwa meneja wa shule.

(3) Nakala ya kila amri iliyo-thibitishwa itapelekwa kwa mtu mwenye jukumu la kumfikisha mtoto huyo katika shule na mtu huyo

ataiwasilisha kwa meneja.

(4) Amri itakuwa ni mamlaka tosha kwa ajili ya kumpokea mtoto katika shule kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu au hadi atakapofikisha umri wa miaka kumi na nane, chochote kitakachotangulia.

Kusimamishwa kwa amri ya shule iliyothibitishwa

125. Utekelezaji wa amri ya shule iliyoidhinishwa, unaweza kusimamishwa ukingojea kukamilika kwa maandalizi ya kumpokea mtoto huyo katika shule ya maadilisho au kutokana na afya yake kuwa dhaifu au kwa sababu yoyote nyingine inayofaa na katika hali hiyo, mahakama inaweza kumweka mtoto huyo katika mahabusi ya watoto au inaweza kuamuru mtoto kuwekwa chini ya himaya ya mtu anayefaa na aliye tayari kuchukua jukumu la uangalizi au inaweza kumuachilia kwa dhamana.

Mamlaka ya kuweka kizuizini

126. Mtoto, akiwa amepokelewa katika shule iliyoidhinishwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii na ambaye wakati anapelekwa au kutoka katika shule hiyo, atachukuliwa kuwa yuko katika uangalizi halali na iwapo atatoroka anaweza kukamatwa bila ya kibali na kurudishwa katika shule hiyo.

Kuongezwa kwa muda wa kuwa kizuizini

127. Endapo meneja au mlezi anaridhika kwamba mtoto ambaye muda wake wa kuwa kizuizini unakaribia kuisha anahitaji uangalizi zaidi au mafunzo anaweza kuomba amri ya mahakama kumweka mtoto huyo kwa kipindi cha ziada kisichozidi mwaka mmoja, isipokuwa, mtoto huyo hatozuiliwa zaidi ya tarehe ambayo atatimiza umri wa miaka kumi na nane.

Mamlaka ya meneja kuwafikisha watu walio katika kizuizi mahakamani

128. Endapo meneja au mlezi wa shule iliyoidhinishwa ataridhika kuwa mtoto aliywekwa katika shule ni mwenye mwenendo wa kitukutu au wa tabia mbaya ambayo haitakiwi kiasi kwamba anatakiwa kubaki katika shule au hairekebiki au kuwa ni mfano mbaya kwa wenzake, meneja huyo au mlezi anaweza, kwa ridhaa ya Bodi, kusababisha mtu huyo kuletwa mbele ya mahakama iliyo na mamlaka katika eneo ambalo shule hiyo ya maadilisho ilipo au mbele ya mahakama iliyotoa amri ya shule ya maadilisho na mahakama inaweza kutoa amri yoyote ambayo ingetolewa kihalali na mahakama ya awali chini ya masharti ya sheria hii na inaweza kufuta kipindi chote au kupunguza sehemu ya kipindi kilichobaki cha kuwa kizuizini ambacho hakijakoma.

- Kuachiliwa au kuhamishwa kutoka katika shule maadilisho
- Muda wa rufaa
- Amri ya Shule ya Maadilisho kuanza kutumika wakati uamuzi wa Mahakama Kuu usubiriwa
- Mamlaka ya kutunga kanuni
129. Meneja au mlezi wa shule iliyothibitishwa kwa ridhaa ya Bodi anaweza-
- (a) kuamuru mtoto yejote ambaye kipindi chake cha kuwa kizuijini kimezidi miezi sita isipokuwa hakijazidi miezi kumi na mbili kuachiliwa;
  - (b) kuamuru mtoto yejote ambaye muda wake wa kuwa kizuijini umeisha kuachiliwa; na
  - (c) kuamuru mtoto yejote kuhamishwa kutoka katika shule moja ya maadilisho kwenda katika shule nyingine.
- 130.-(1) Kila rufaa dhidi ya amri au hukumu iliyotolewa au kuamuliwa na Mahakama ya Watoto chini ya masharti ya Sheria hii itawasilihwa ndani ya siku kumi na nne kutoka tarehe ambayo amri au hukumu inayokatiwa rufaa ilitolewa.
- (2) Mahakama Kuu, inaweza, kwa nia njema, kukubali rufaa nje ya muda.
- (3) Pale ambapo hakuna rufaa iliyowasilishwa dhidi ya amri ya shule ya maadilisho iliyotolewa na Mahakama ya Wilaya chini ya masharti ya Sheria hii ndani ya muda uliyoelekezwa, nakala ya amri hiyo pamoja na mwenendo wa kesi utawasilihwa katika Mahakama Kuu na Mahakama Kuu inaweza, katika kutekeleza mamlaka yake ya kurejea upya kesi, kutoa amri kwa kadri itakavyoona inafaa.
131. Bila kujali kitu chochote katika Sehemu hii, amri ya shule ya maadilisho haitosimamishwa kwa sababu tu kwamba hakuna amri ya Mahakama Kuu iliyopokelewa katika kutekeleza mamlaka yake ya rufaa au ya kurejea upya, kesi, haijapokelewa isipokuwa kwamba mtoto anayehusika yupo chini ya uangalizi wa mtu anayefaa au ameachiliwa kwa dhamana.
- 132.-(1) Waziri mwenye dhamana na ustawi wa jamii anaweza kutunga kanuni kwa utekelezaji bora wa majukumu na masharti ya Sheri hii na, bila kuathiri ujumla wa yafuatayo, zikielezea madhumuni yafuatayo-
- (a) utawala, udhibiti na nidhamu na uchumi wa ndani wa shule za maadiliisho na nyunba za makazi;
  - (b) usajili wa watoto walioko katika shule za maadilisho;
  - (c) ziara za wazazi, walezi au ndugu wa mtoto;

(d) shule, mafunzo na maadilisho ya watoto.

(2) Sheria zilizotungwa chini ya kifungu hiki zinaweza kutumika kwa shule za maadilisho au nyumba za makazi au kwa shule maalum ya maadilisho au mahabusi za watoto.

**SEHEMU YA KUMI NA MOJA**

**MATUNZO YA KITAASISI**

*(a) Makazi au Taasisi zilizothibitishwa*

Uidhinishaji  
wa makao  
yaliyothi-  
bitishwa

133.-(1) Serikali inaweza kuanzisha makazi au taasisi zilizothibitishwa kwa ajili ya matunzo ya watoto katika maeneo ambayo Kamishna anaweza kuamua.

(2) Mtu yejote anaweza uanzisha na kuendesha makao yaliyothibitishwa au taasisi kwa ajili ya matunzo ya watoto kwa kuzingatia idhini ya Kamishna.

(3) Ombi la kuidhinishwa kwa makao yaliyothibitishawa au taasisi litafanywa kwa namna ilioelekezwa na kuwasilishwa kwa Kamishna.

- (a) usajili wa watoto walio katika shule za maadilisho;
- (b) ziara za wazazi, mlezi au ndugu wa mtoto huyo;
- (c) elimu, mafunzo na urekebishaji wa watoto.

(2) Kanuni zilizotengenezwa chini ya kifungu hiki zinaweza kutumika shule zote za maadilisho na mahabusi za watoto au shule yoyote mahsusni ya maadilisho na mahabusi za watoto.

(4) Kamishna ataagiza makao yaliyothibitishwa au taasisi kukaguliwa na Afisa Ustawi wa Jamii na kama nyumba hiyo inakidhi masharti ya viwango vinavyohitajiwa itadhibitishwa kwa notisi katika Gazeti la Serikali.

(5) Baada ya kupata idhini ya Kamishna, makao yaliyothibitishwa au taasisi iliyoidhinishwa itapewa leseni ya kuendesha shughuli leseni ambayo itatolewa na Kamishna.

(6) Masharti ya kifungu kidogo cha (5) hayatatumika kwa makao yaliyothibitishwa au taasisi za Serikali.

(7) Makao yaliyothibitishwa au taasisi ya maadilisho binafsi

iliyokuwepo kabla yakuanza kutumika kwa Sheria hii, itawasilisha maombi kwa Kamishna kwa idhini yake na itapewa leseni ndani ya kipindi cha miezi sita kutokea kuanza kutumika kwa Sheria hii.

(8) Kwa madhumuni ya Sehemu hii Ndogo “makao yaliyothibitishwa” na “taasisi” zitajumuisha-

- (a) makao ya watoto;
- (b) nyumba ya mahabusi;
- (c) shule ya maadilisho;
- (d) kituo cha dharura; na
- (e) taasisi nyingine yoyote iliyoteuliwa kwa matumizi hayo na Kamishna.

(9) Makao yaliyothibitishwa na taasisi zinazorejewa chini ya kifungu kidogo cha (8) kwa notisi zitachapishwa katika Gazeti la Serikali.

Ufuatiliaji  
wa makao na  
taasisi

134.-(1) Ilikuwa ni jukumu la Kamishna kufuatilia na kusimamia makao yaliyoidhinishwa au taasisi.

(2) Kwa madhumuni ya kuendeleza ustawi wa watoto, kila makao na taasisi iliyothibitishwa itaunda kamati ya watu wanaofaa isiyopungua wanne kwa ajili ya kuangalia uendeshaji na usimamizi wa ujumla wa ustawi na maendeleo ya watoto.

(3) Kamishna anaweza kukasimu kwa mtu yeyote yule katika utumishi wa umma madaraka ya kutekeleza wajibu uliyo chini ya kifungu kidogo cha (1).

(4) Waziri mwenye dhamana na masuala ya Ustawi wa Jamii anaweza kutengeneza kanuni zitakazoainisha muundo, sifa na masuala mengine yoyote yanayohusiana na kamati iliyoundwa chini ya kifungu kidogo cha (2).

Mamlaka ya  
Kamishna  
kutoa  
maelekezo  
kwa makao

135. Kamishna anaweza kutoa amri na maelekezo kwa makazi au taasisi iliyothibitishwa, kama itakavyohitajika, kwa madhumuni ya kuendeleza maendeleo ya mtoto.

Ukaguzi wa  
makao

136. Kamishna anaweza kuelekeza ukaguzi wa makazi au taasisi iliyothibitishwa kufanywa na Afisa Ustawi wa Jamii katika muda wowote ili kuhakikisha kuwa makao au taasisi hizo zilizothibitishwa zinawekwa katika viwango vinavyotakiwa.

Kupokelewa  
kwa watoto  
katika makao  
yaliyothibiti-  
shwa

137.-(1) Mtoto anaweza kupokelewa katika makazi au taasisi  
iliyothibitishwa-

- (a) wakati uamuzi wa mahakama kuhusu matunzo na ulinzi wa mtoto unasubiriwa;
- (b) kwa mapendekezo ya Afisa Ustawi wa Jamii ambaye ameamua kuwa makao hayo au taasisi iliyothibitishwa ni sehemu inayofaa zaidi kwa mtoto huyo; au
- (c) kwa ridhaa ya Afisa Ustawi wa Jamii, iwapo mtoto huyo ni yatima na huduma ya uangalizi wa kifamilia na huduma za malezi ya kambo hayapo.

(2) Pale ambapo makao au taasisi iliyothibitishwa imeshindwa kuzingatia viwango vinavyohitajika, leseni yake ya uendeshaji inaweza kufutwa au kusimamishwa na Kamishna na Kamishna ataandaa mpango kwa ajili ya watoto katika makao au taasisi iliyothibitishwa.

(3) Litakuwa ni jukumu la wafanyakazi wa makao au taasisi iliyothibitishwa, Afisa Ustawi wa Jamii au mtu mwagine yeoyote mwenye jukumu la kumtunza mtoto, kumsaidia mtoto huyo kuweza kuunganishwa na wazazi wake, walezi au ndugu.

(4) Baada ya mtoto kurudishwa katika familia yake, mlezi, meneja na Afisa Ustawi wa Jamii atamtembelea mara kwa mara mtoto na familia yake ili kuhakikisha kuwa maslahi ya mtoto yanaendelezwa.

(5) Endapo mtoto atashindwa kurudi kwa wazazi wake au kwenda kwa walezi wa kambo, mtoto atahamasishwa na kusaidiwa na mlezi, meneja na Afisa Ustawi wa Jamii kuwa huru na kujitegemea.

(6) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (5) mtoto hatatakiwa kuondoka katika makao au taasisi iliyothibitishwa kama yupo chini ya umri wa miaka kumi na nane.

Jukumu la  
ulezi kwa  
wafanyakazi  
wa makao  
yaliyothibiti-  
shwa

138.-(1) Mtoto anapokuwa yupo katika makazi au taasisi iliyothibitishwa wafanyakazi wa makao au taasisi iliyothibitishwa watakua na jukumu la ulezi kwa mtoto ili kuhakikisha kuwa haki za mtoto chini ya sheria hii zinalindwa.

(2) Bila kujali kifungu kidogo cha (1), wazazi, walezi au ndugu wa mtoto aliywekwa katika makao yoyote yaliyothibitishwa au

taasisi watachangia malezi katika makao au taasisi iliyothibitishwa ili kulinda na kukuza ustawi wa mtoto kwa kumtembelea mtoto na kulinda maslahi yake.

(3) Jukumu la ulezi wa mtoto katika makao yaliyothibitishwa au taasisi itajumuisha maombi kwa mahakama ili kulinda maslahi ya mtoto pale inapobidi.

Uwezo wa  
mahakama  
kuamuru  
uchangiaji

139.-(1) Mahakama inaweza kuamuru mzazi, mlezi au ndugu wa mtoto ambaye yupo katika makao yaliyothibitishwa au taasisi kuchangia katika matunzo ya mtoto katika makao yaliyothibitishwa au taasisi.

(2) Kiasi chochote kitakachochangiwa kitakuwa ni cha kuridhisha na kinaweza kubadilishwa na mahakama iwapo kuna mabadiliko katika mazingira ya mchangiaji.

Kufutwa kwa  
leseni ya  
makao  
yaliyothibiti-  
shwa

140.-(1) Endapo Kamishna anazo sababu za msingi za kuamini kwamba-

- (a) majengo ya makao ya watoto hayafai tena kutumika kama shule ya maadilisho;
- (b) makao ya watoto yapo katika mazingira yasiyo safi na salama;
- (c) vifaa vilivyopo kwa ajili ya afya au ustawi wa watoto waliopokelewa katika makao ya watoto havitoshelezi; au
- (d) mwenye leseni ameshindwa kuzingatia kanuni zozote zinazo simamia uendeshaji na usimamizi wa makao yaliyothibitishwa,  
ataifuta leseni hiyo.

(2) Kamishna, baada ya kufuta leseni chini ya kifingu kidogo cha (1), ataandaa utaratibu mbadala wa watoto wanaoishi katika makao hayo.

Haki ya  
kusikilizwa

141.-(1) Kamishna anaweza, baada ya kumpa mwenye leseni fursa ya kusikilizwa au kutoa taarifa kwa notisi ya maandishi akimtaka kabla ya tarehe iliyoinishwa katika notisi kurekebisha mapungufu yaliyoinishwa katika notisi kwa kiwango cha kumridhisha Kamishna.

(2) Endapo mwenye leseni atashindwa kukidhi masharti ya notisi

iliyotolewa katika kifungu kidogo cha (1), Kamishna baada ya kumtaka mwenye leseni kutoa sababu kwa nini leseni yake isifutwe, anaweza kuifuta leseni hiyo.

Sababu ya  
maamuzi  
kutolewa

142. Kamishna, kwa maombi ya mtu ambaye ombi lake la kupatiwa au kupatiwa upya leseni limekataliwa au mtu ambaye leseni yake imefutwa, atamfahamisha mtu huyo mara moja kwa maandishi sababu za maamuzi yake.

Makao  
yaliyotibithi-  
shwa na  
uasili

143.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, mtoto aliye katika makao yaliyothibitishwa au taasisi atatolewa kwa ajili ya kuasiliwa kama itakuwa ni kwa maslahi yake.

(2) Maamuzi ya kuasiliwa kwa mtoto katika makao yaliyothibitishwa au taasisi yatachukuliwa na Kamishna kwa kushauriana na uongozi wa makao hayo.

(3) Uasili chini ya kifungu kidogo cha (2), utazingatia utaratibu wa uasili ulioainishwa katika Sheria hii.

Mama aliye  
gerezani  
pamoja na  
mtoto

144.-(1) Pale ambapo mama atakuwa gerezani na mtoto wake katika mazingira yoyote, hatua zote zitachukuliwa na uongozi wa magereza kuhakikisha kuwa mtoto anapata matunzo yanayohitajika katika namna inayostahili, mlo kamili, virutubisho na huduma ya afya pamoja na chanjo.

(2) Uongozi wa magereza utamfahamisha Afisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya kuhusu mtoto aliye gereani na mama yake na ambaye ameshaacha kunyonya.

(3) Endapo Afisa Ustawi wa Jamii amepokea taarifa kutoka katika uongozi wa gerezani, ataamua sehemu stahili ya kumweka mtoto huyo, ambayo inaweza kuwa-

- (a) mzazi ambaye hayuko gerezani;
- (b) ndugu;
- (c) mlezi; au
- (d) mtu anayefaa kulea.

(4) Iwapo watu waliotajwa chini ya kifungu kidogo cha (3) wanakosekana, Afisa Ustawi wa Jamii ataagiza mtoto huyo apelekwe katika makao yaliyothibitishwa hadi hapo mama yake atakapoachiliwa kutoka gerezani.

Waziri  
kutunga

145. Waziri mwenye dhamana ya Ustawi wa Jamii anaweza, kwa

kanuni za makao kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya watoto, kutengeneza kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora na uendelezaji viwango vya makao yaliyothibitishwa, taasisi, vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na vituo vya kulelea watoto wachanga.

Makosa na adhabu 146.-(1) Adhabu ya ukiukwaji wa haki za mtoto na jukumu la ulezi zilizoainishwa chini ya Sheria hii, zitamhusu pia meneja, mlezi, mmiliki wa leseni na mtu ye yeyote katika makao yaliyothibitishwa au taasisi ambaye atashindwa kuzingatia haki za mtoto.

(2) Mtu ye yeyote ambaye-

- (a) anaendesha makao yaliyothibitishwa au taasisi bila ya leseni iliyotolewa na Kamishna;
- (b) anaendelea kuendesha makao yaliyothibitishwa au taasisi kwa kukiuka masharti ya sehemu hii; au
- (c) anamzuia Afisa Ustawi wa Jamii kufanya ukaguzi chini ya Sehemu hii,

anatenda kosa na atakapotiwa hatiani atalipa faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi milioni kumi au kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja au vyote kwa pamoja; na iwapo ataendelea kutenda kosa, atalipa faini isiyopungua shilingi laki moja kwa kila siku ambayo kosa linaendelea kufanyika.

*(b) Vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na vituo vya kulelea watoto wachanga*

Maombi ya kuendesha kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au kituo cha kulelea watoto wachanga yatawasilishwa na muombaji kwa Kamishna.

(2) Maombi hayo yatafanywa katika namna itakavyo elekezwa na yataambatana na ada kama itakavyo elekezea.

(3) Baada ya kupokelewa kwa maombi ya kusajiliwa kwa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au kituo cha kulelea watoto wachanga, Kamishna ataagiza ukaguzi wa majengo na mazingira kufanyika, na anaweza kukisajili kituo hicho kuwa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au kituo cha kulelea watoto wachanga iwapo ataridhika kuwa-

- (a) majengo na mazingira ya kuendesha kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au kituo cha kulelea watoto wachanga yanafaa kwa idadi maalum ya watoto;
- (b) mwombaji ana uwezo wa kifedha na rasilimali watu wa kutosha kwa ajili ya kutunza majengo na mazingira hayo kwa

mujibu wa matakwa ya vituo vya kulelea watoto wadogo mchana kituo cha kulelea watoto wachanga kama yalivyoainishwa katika kanuni;

- (c) mwombaji anaweza kuweka katika majengo na mazingira vifaa vyote muhimu vya uendeshaji wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au kituo cha kulelea watoto wachanga;
- (d) umiliki wa jengo na mazingira hauna mgogoro wowote mbele ya mahakama yoyote au mamlaka yoyote nyingine.

(4) Katika kuamua iwapo jengo au mazingira linafaa kwa usajili au la, Kamishna atazingatia programu iliopendekezwa kwa ajili ya matunzo na ulezi kwa watoto, hususan -

- (a) iwapo programu zitaendeshwa katika majengo au mazingira hayo zinaweza zikahamasisha maendeleo ya watoto wanaohudhuria katika kituo hicho kuwa watu wenyenidhamu na tabia nzuri;
- (b) programu za vituo vya kulelea watoto wadogo mchana au kituo cha kulelea watoto wachanga zitakuwa imara kwa kuwawezesha watoto kukua katika afya njema nakuwa raia wema; na
- (c) vifaa vya kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au kituo cha kulelea watoto wachanga kinachopendekezwa vitakuwa vinafaa kwa kuwandaa watoto kuingia katika elimu ya awali.

(5) Afisa Ustawi wa Jamii atakagua vituo vya kulelea watoto wadogo mchana au kituo cha kulelea watoto wachanga na baada ya kuridhika kuwa matakwa ya Sheria hii yamezingatiwa, ataidhinisha maombi hayo.

(6) Endapo Kamishna anapitisha maombi chini ya kifungu hiki, atatoa kwa mwombaji cheti cha usajili kuhusiana na jengo au mazingira vilivyoasajiliwa ambayo itakuwa na maelezo sahihi ya jengo au mazingira hayo na maelezo mengine kama itakavyoelezewa.

(7) Kituo chochote cha kulelea watoto mchana au kituo cha kulelea watoto wachanga ambacho kinaendesha shughuli zake bila ya usajili chini ya kifungu hiki kitafungwa.

(8) Kabla ya kufungwa chini ya kifungu kidogo cha (8), Kamishna atatoa notisi ya siku kumi na nne.

Katazo la  
baadhi ya

148.-(1) Mtu ambaye ametiwa hatiani kwa kosa dhidi ya watoto au kosa lolote la makosa ya kujamiiiana hatoajiriwa katika kituo cha

watu  
kuendesha  
vituo vya  
kulelea  
watoto  
wadogo  
mchana au

kulelea watoto wadogo mchana au kituo cha kulelea watoto wachanga.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidigo cha (1), Kamishna atahakikisha kuwa meneja, mlezi au mtu mwininge yeoyote anayeendesha au kufanya kazi katika kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au kituo cha kulelea watoto wachanga anafanyiwa upekuzi na Kamishna.

Usajili wa  
wamiliki wa  
vituo

149.-(1) Mtoto aliye katika kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au kituo cha kulelea watoto wachanga atakuwa chini ya umri wa miaka mitano.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (3), maombi ya kusajili umilki au umeneja wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au creches yatapelekwa kwa Kamishna katika namna iliyoelekezwa na yataambatana na ada zilizoainishwa.

(3) Kamishna anaweza kukubali maombi ya kusajiliwa chini ya kifungu hiki iwapo tu ameridhika kuwa -

- (a) jengo au mazingira ambayo muombaji anapendekeza kuanzisha kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au kituo cha kulelea watoto wachanga yamekaguliwa na kuandikishwa;
- (b) mwombaji ana rasilimali fedha za kutosha kiasi cha kumuwezesha kupata wafanyakazi wanaofaa na kutoa huduma kwa watoto, kwa kuzingatia viwango vinavyotakiwa kwa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au kituo cha kulelea watoto wachanga;
- (c) mwombaji hajapoteza sifa kwa njia yoyote ili kuweza kusajiliwa au mtu ambaye usajili wake umefutwa hapo awali; na
- (d) mwombaji anakidhi kwa namna zote matakwa mengine yoyote ambayo yanaweza kuelekezwa kwa wamiliki au mameneja wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana ua kituo cha kulelea watoto wachanga.

(4) Kamishna atatoa cheti stahili kwa mtu aliyesajiliwa, kitakachokuwa na maeleo kama Waziri mwenye dhamana ya Ustawi wa Jamii atakavyoolekeza.

Rejesta ya  
kituo cha

150.-(1) Afisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya ataagiza kuanzishwa na kutunzwa kwa rejesta tofauti katika namna iliyoelekezwa katika

kulelea  
watoto  
wadogo  
mchana na  
kituo cha  
kulelea  
watoto  
wachanga

fomu maalum kwa kila kituo cha kulelea watoto wadogo mchana na kituo cha kulelea watoto wachanga kilichosajiliwa pamoja na wamilki na mameneja wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na kituo cha kulelea watoto wachanga waliosajiliwa.

(2) Kila rejestra itakuwa na jina la kila kituo cha kulelea watoto wadogo mchana na kituo cha kulelea watoto wachanga na kila mmiliki au meneja wa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana na kituo cha kulelea watoto wachanga aliyesajiliwa chini ya Sheria hii pamoja na maelezo mengine yanayohusu kituo cha kulelea watoto wadogo mchana na mmiliki wake au meneja kilichosajiliwa na msajili anaweza kufuta au kurekebisha maelezo yoyote yale kadri mazingira yatakavyohitaji.

(3) Msajili, japo mara moja kila mwaka, ataagiza kutangazwa katika Gazeti la Serikali au gazeti jingine lolote linalochapishwa na kusambazwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, orodha ya vituo vyote vya kulelea watoto wadogo mchana na kituo cha kulelea watoto wachanga ambavyo usajili wake umefutwa na vile ambavyo vimesajiliwa kwa mara ya kwanza.

Idara  
kukagua

151.-(1) Kamishna atakagua majengo na mazingira, vitabu, mahesabu na kumbukumbu nyingine za kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au kituo cha kulelea watoto wachanga, makao yaliyothibitishwa au taasisi japo mara moja katika kila miezi sita na atawasilisha taarifa ya ukaguzi huo kwa Waziri mwenye dhamana na ustawi wa jamii na nakala kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya watoto.

(2) Endapo ukaguzi unaonesha kuwa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au kituo cha kulelea watoto wachanga hakiendeshwi kiufanisi kwa maslahi ya watoto, Kamishna atafuta kibali na mmilki au muendesha kituo ataamuliwa kufanya marekebisho ya mapungufu katika muda ulioelekezwa.

(3) Endapo mmilki au muendesha kituo anashindwa kufanya marekebisho ya mapungufu ndani ya muda ulioelekezwa, kibali kitafutwa.

(4) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (2), iwapo Kamishna amefuta leseni, atafanya au kuagiza kufanywa maombi ya amri ya

mahakama ya kuhamishwa watoto pamoja na kumbukumbu husika kwenda katika kituo kingine cha kulelea watoto mchana au kituo cha kulelea watoto wachanga au makao yaliyothibitishwa au taasisi, mara moja.

(5) Kamishna, badaa ya ukaguzi kuonyesha kuwa kituo cha kulelea watoto wadogo mchana, kituo cha kulelea watoto wachanga au makao yaliyothibitishwa ambayo leseni yake ilifutwa, na yamerekebisha mapungufu, atatoa usajili upya; isipokuwa usajili huo mpya utafanyika katika kipindi cha miaka miwili baada ya ufutwaji.

**SEHEMU YA KUMI NA MBILI**  
**MASHARTI MENGINEYO**

Sheria ndogo  
na miongozo

152. Mamlaka ya Serikali za Mitaa inaweza, kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana na masuala ya ustawi wa jamii, kutoa sheria ndogo na miongozo kadri itakavyoamua kwa ajili ya uendeshaji wa makao yaliyothibitishwa, taasisi, vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na vituo vya kulelea watoto wachanga vilivyoko ndani ya wilaya yake.

Maelekezo

153.-(1) Waziri mwenye dhamana na ustawi wa jamii ataanzisha vituo vya mafunzo kwa wafanyakazi wanaotunza watoto wanaokusudia kufanya kazi katika makao yaliyothibitishwa, taasisi na vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na vituo vya kulelea watoto wachanga.

(2) Waziri, anaweza, kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana na ustawi wa jamii na Waziri mwenye dhamana na elimu, kutoa maelekezo ya kisera kama atakavyoona inafaa kwa ajili ya uendeshwaji wa makao yaliyothibitishwa, taasisi na vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na vituo vya kulelea watoto wachanga.

Waendeshaji  
waliopo

154. Mtu yeьте anayemilki au kuendesha makao yaliyothibitishwa, taasisi, kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au kituo cha kulelea watoto wachanga kabla ya kuanza kutumika kwa sheria hii, na anakusudia kuendelea kuendesha makao hayo yaliyothibitishwa, taasisi, kituo cha kulelea watoto wadogo mchana au vituo vya kulelea watoto wachanga, ataomba kibali kwa

Kamishna ndani ya miezi sita tangu kuanza kutumika kwa Sheria hii.

Makosa na  
adhabu

155. Mtu yeoyote ambaye -

- (a) anaendesha kituo cha kulelea watoto wadogo mchana bila ya leseni au kibali kilichotolewa na Kamishna;
- (b) anaendelea kuendesha makao yaliyothibitishwa kinyume na Sheria hii; au
- (c) anamzuia Afisa Ustawi wa Jamii kuendesha ukaguzi chini ya Sheria hii,

anatenda kosa na atakapotiwa hatiani atalipa faini isiyopungua shilingi milioni mbili na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichozi mwaka mmoja au vyote kwa pamoja, atalipa faini ya ziada isiyozidi shilingi laki moja kwa kila siku ambayo kosa linaendelea kufanyika.

Rufaa

156. Isipokuwa kama imeelezewa vinginevyo katika sheria nyingine, mtu ambaye hajaridhika na uamuvi wa Kamishna kwa-

- (a) kukataa kuruhusu au kutoa leseni au kibali upya;
- (b) kuifuta leseni au kibali;
- (c) kukataa kusajili kituo cha kulelea watoto wadogo mchana; au
- (d) kufuta usajili,

anaweza, ndani ya siku thelathini baada ya kupokea notisi ya uamuvi wa Kamishna, kukata rufaa kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya ustawi wa jamii dhidi ya uamuvi huo.

Kanuni

157. Waziri mwenye dhamana na ustawi wa jamii, kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana na masuala ya watoto, anaweza kuandaa kanuni zitakaoainisha-

- (a) malezi na ulinzi wa watoto; utaratibu wa kuwapokea na kuwaondoa watoto kutoka katika makao yaliyothibitishwa na taasisi;
- (b) uwekwaji katika malezi ya kambo;
- (c) uasili;
- (d) ajira kwa watoto;
- (e) uanaganzi;
- (f) watoto kuambatana na mzazi, mlezi au ndugu aliyelazwa hospitali kwa muda wa zaidi ya miezi sita;
- (g) uasili wa wazi;
- (h) maswala yaliyoainishwa chini ya kifungu cha 6, 7 na 8;
- (i) makao yaliyothibitishwa na taasisi; na
- (j) kwa ujumla wake ukuzaji na uendelezaji wa madhumuni ya

Sheria hii.

Katazo la  
jumla

- 158.-(1) Mtu hata-
- (a) tenda au kuagizwa kutendwa ukeketaji kwa mtoto;
  - (b) chapisha, kutengeneza, kuonyesha au kuagiza kuchapishwa, kuendeshwa au kuonyeshwa picha au taswira ya mtoto au mtoto aliyefariki ilioonyesha ukatili au katika pozzi za ngono;
  - (c) kumtumia mtoto katika maonyesho ya harusi, maonyesho ya mitindo ya nguo au maonyesho mengine yoyote yanayofanana na hayo wakati wa usiku;
  - (d) chapisha au agiza kuchapishwa taarifa yoyote ambayo inaathiri maslahi ya mtoto;
  - (e) kulazimisha mtoto aliyeasiliwa au mtoto aliye chini ya malezi ya kambo kubadili dini yake ya kuzaliwa; au
  - (f) kutumia au agiza kutumika au kumhusisha mtoto aliye katika makao yaliyothibitishwa au taasisi kwa ajili ya kuomba omba au kwa ajili ya faida binafsi; na
  - (g) tumia vibaya msaada au aina nyingine ya msaada uliyolengwa katika kusaidia au kutunza watoto katika taasisi.
- (2) Mtu yeyote atakayekiuka masharti yoyote ya kifungu kidogo cha (1), anatenda kosa na atakapotiya hatiani atalipa faini isiyopungua shilingi laki tano au kifungo cha miezi sita au vyote kwa pamoja.

Adhabu ya  
jumla

159. Mtu yeyote atakayekiuka masharti yoyote ya Sheria hii ambayo hakuna adhabu maalum iliyotolewa anatenda kosa na atakapotiya hatiani atalipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

Kufutwa na  
masharti ya-  
nayoendelea  
Sura Na.13,  
16, 180, 298  
na 335

- 160.-(1) Sheria zifuatazo zimefutwa-
- (a) Sheria ya Matunzo ya Watoto;
  - (b) Sheria ya Uasili;
  - (c) Sheria ya Vituo vya kulelea watoto wadogo mchana;
  - (d) Sheria ya Watoto na Vijana; na
  - (e) Sheria ya Makao ya Watoto.

(2) Bila kujali kufutwa kwa Sheria zilizoainishwa katika kifungu kidogo cha (1)-

- (a) watu wote waliyo na mamlaka chini ya Sheria zilizofutwa kusimamia majukumu yoyote yaliyoainishwa katika Sheria hii, watachukuliwa kuwa na mamlaka ya kusimamia majukumu sawa na hayo kama yalivyoainishwa chini ya Sheria hii.

- (b) leseni zote na vibali vilivyotolewa chini ya masharti ya sheria zilizofutwa zitachukuliwa kuwa zimetolewa chini ya Sheria hii na zitakuwa na nguvu hadi hapo zitakapobadilishwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii; na
- (c) kanuni zote zilizotengenezwa chini ya masharti ya sheria zilizofutwa, zitachukuliwa kuwa zimetengenezwa chini ya Sheria hii na zitaendelea kuwa na nguvu mpaka zitakapobadilishwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii; na
- (d) amri zote, notisi, sheria ndogo, maelekezo yaliyotolewa au kitu kingine kilichotolewa au kutengenezwa na mtu aliyepewa mamlaka hayo na afisa aliyepewa mamlaka kutoa au kutengeneza amri, notisi, sheria ndogo, maelekezo yaliyotolewa chini ya sheria zilizofutwa zitachukuliwa kuwa zimetengenezwa chini ya Sheria hii na zitaendelea kuwa na nguvu na hadi hapo zitakaporekebishwa au kuondolewa chini ya Sheria hii.

(3) Ada zozote zilizotozwa na vyeti vilivyotolewa chini ya masharti ya sheria zilizofutwa, bila kujali kufutwa kwa sheria tajwa hapo awali, zatabaki kuwa na nguvu kama vile ni ada zilizotozwa au vyeti vilivyotolewa chini ya Sheria hii hadi hapo zitakapoondolewa au kubadilishwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

#### **SEHEMU YA KUMI NA TATU**

##### **MAREKEBISHO YATOKANAYO**

###### *(a) Sehemu Ndogo ya Kwanza*

Muundo  
Sura 29

Marekebiso  
ya kifungu  
cha 2

161. Sehemu hii itasomwa kwa pamoja na Sheria ya Ndoa, ambayo itajulikana kama “Sheria Kuu”.

162. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 2 kwa -
- (a) kufuta tafsiri ya istilahi “Mtoto” na kuibadilisha na istilahi ifuatayo:  
“Mtoto” maana yake ni mtu aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane”;
  - (b) kufuta:
    - (i) marejeo yote yanayohusiana na tafsiri ya istilahi “mchanga” na “mtoto mchanga”;
    - (ii) maneno “watoto wachanga” na “mchanga” popote yatakapoonekana katika Sheria hiyo na kuyabadilisha na maneno “watoto” na “mtoto” kama hali itakavyokuwa.

- Marekebisho ya kifungu cha 17

(a) kuingiza alama ya kituo baada ya alama ya mkato ambayo inaonekana baada ya neno “msimamizi”; na

(b) kufuta fungu “isipokuwa katika hali nyingine yoyote, au kama watu hao wamefariki, haitahitaji kibali”.

Marekebisho ya kifungu cha 64

163. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 17 kwa -

165. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 64(1) kwa kufuta neno “mchanga” linaloonekana kati ya maneno “ya” na “watoto”.

*(b) Sehemu ndogo ya Pili*

Muundo Sura ya 35

167. Sehemu hii ndogo itasomeka kwa pamoja na Sheria ya Elimu, ambayo itafahamika kama “Sheria Kuu”.

Marekebisho ya kifungu cha 35

168. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 35 kwa kuingiza mara baada ya kifungu kidogo cha (1), fungu lifuatatalo:

“1A. Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), hakuna mtoto wa umri wa miaka saba au zaidi atakayekataliwa kuandikishwa katika shule.”

Marekebisho ya kifungu cha 59

169. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 59 kwa kuongeza kifungu kipyta cha 59A kama ifuatavyo:

“Wajibu	59A.-(1) Kila mwalimu, fundi stadi, fundi
wa	mchundo na mkufunzi atakuwa na wajibu wa
kutoa	jumla wa kutoa taarifa ya ushahidi au malalamiko
taarifa	ya unyanyasji kwa mtoto yanayofanywa na mtu
	yeoyote kwa Afisa Ustawi wa Jamii anayehusika.

(2) Kila mwalimu, fundi stadi, fundi mchundo na mkufunzi atakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa maslahi ya mwanafunzi yanapewa kipaumbele.

Marekebisho ya kifungu cha 60

170. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 60 kwa -

(a) kuongeza aya mpya ya (k) kama ifuatavyo:

“(k) anayempa ujauzito mwanafunzi wa shule ya msingi au shule ya sekondari”;

(b) kwa kubadilisha maneno “shilingi elfu kumi” na maneno “miezi sita” kwa maneno “shilingi laki tano” na “miaka mitatu” kama itakavyokuwa.

(c) *Sehemu ndogo ya Tatu*

Muundo  
Sura ya 366

171. Sehemu hii Ndogo itasomeka kwa pamoja na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, ambayo itajulikana kama “Sheria Kuu”.

Marekebisho  
ya kifungu  
cha 5

172. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 5 kwa-

- (a) katika kifungu kidogo cha 6(a) kwa kuongeza maneno “na mafunzo” katikati ya maneno “Ajira” na “ya”.
- (b) kwa kuongeza fungu lifuatalo-  
“(9) Bila kuathiri masharti ya kifungu hiki, kila mwajiri atahakikisha kwamba kila mtoto anayeajiriwa kihalali chini ya Sheria hii analindwa dhidi ya ubaguzi au matendo yenye madhara kwa mtoto kwa kuzingatia umri na uwezo na watoto kuelewa.

Muundo  
Sura ya 16

173. Sehemu hii ndogo itasomeka pamoja na Kanuni za Adhabu, ambayo itajulikana kama “Sheria Kuu”.

Marekebisho  
ya kifungu  
cha 5

174. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 5 kwa kuongeza kifungu kipyta kama ifuatavyo-  
“4 Mtu yejote aliye chini ya umri wa miaka kumi na mbili ambaye atatenda kitendo au kuacha kutenda kitendo ambacho ni kinyume na Sheria atashughulikiwa chini ya Sheria ya mtoto ya mwaka 2009”.

Marekebisho  
ya kifungu  
cha 17

175. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 17 kwa kuongeza matamshi yafuatayo mara baada ya neno “kosa” linaloonekana mwishoni mwa kifungu hicho kama ifuatavyo “isipokuwa kama mkosaji ni mtoto”.

Marekebisho  
ya kifungu  
cha 130

176. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 130(3)(c) kwa kuingiza maneno yafuatayo “shule, kituo cha kulelea watoto wadogo mchana, makao ya watoto au taasisi nyingine yoyote, shirika au wakala pale ambapo kuna wajibu wa kutunza” katikati ya maneno “hosipitali” na “anachukua”.

Marekebisho  
ya kifungu  
cha 131

177. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 131 kwa-

- (a) katika kifungu kidogo cha 2(c), kwa kufuta matamshi “kifungo cha maisha” kwa mujibu wa kifungu kidogo

cha (1)”na kukibadilisha na matamshi “miaka mitano” pamoja na adhabu ya viboko”

- (b) katika kifungu kidogo cha (3), kwa kufuta neno “yeyote” na kulibadilisha kwa maneno “mtu mwingine yeyote mbali na mtu aliyerejewa chini ya kifungu kidogo cha (2)”.

Marekebisho  
ya kifungu  
cha 138

178. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 138 kwa -  
(a) kufuta maneno “kumi na tano” na kuyabdalisha na maneno “kumi na nane”, popote yanapoonekana katika kifungu hicho;
- (b) kufuta kifungu kidogo cha (6).

Marekebisho  
ya kifungu  
cha 138B

179. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 138B kwa -  
(a) kwa kubadilisha kifungu cha “138B” kuwa cha “138B.(1)”.  
(b) kufuta maneno “tano” na “miaka ishirini” na kuyabdalisha na maneno “kumi na tano” na “miaka thelathini bila ya kuwepo kwa fani”;
- (c) kuongeza kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

(2) Mahakama inaweza, kwa kuongezea, kuamuru kulipwa kwa fidia ya kiasi chochote cha fedha kwa muathirika”.

Marekebisho  
ya kifungu  
cha 138C

180. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 138C(2)(b) kwa kufuta maneno “kumi na tano” na kuyabdalisha na maneno “kumi na nane”.

Marekebisho  
ya kifungu  
cha 141

181. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 141 kwa-  
(a) kufuta maneno “chini ya umri wa miaka kumi na tano”;  
(b) kufuta kifungu hicho.

Marekebisho  
ya kifungu  
cha 142

182. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 142 kwa kufuta maneno “kumi na sita” popote yanapoonekana katika kifungu hicho na kuyabdalisha na maneno “kumi na nane”.

Marekebisho  
ya kifungu  
cha 144

183. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 144(3) (a) na (b) kwa kufuta maneno “kumi na sita na kuyabdalisha kwa maneno “kumi na nane”.

- Marekebisho ya kifungu cha 147      184. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 147 kwa kufuta neno “mke”.
- Marekebisho ya kifungu cha 154      185. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 154 kwa kufuta neno “kumi” na kulibadilisha kwa maneno “kumi na nane”.
- Marekebisho ya kifungu cha 156      186. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 156(1) kwa kufuta maneno “kumi na nne” na kuyabadilisha na maneno “kumi na nane”.
- Marekebisho ya kifungu cha 160      187. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 160 kwa kufuta maneno “kumi” na kuyabadilisha kwa maneno “kumi na nane”.
- Marekebisho ya kifungu cha 166      188. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 166 kwa kufuta maneno “kumi na nne” na kuyabadilisha kwa maneno “kumi na nane”.
- Marekebisho ya kifungu cha 167      189. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 167 kwa kufuta maneno “kumi na nne” na kuyabadilisha kwa maneno “kumi na nane”.
- Marekebisho ya kifungu cha 169      190. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 169 kwa kufuta maneno “kumi na nne” na kuyabadilisha kwa maneno “kumi na nane”.
- Marekebisho ya kifungu cha 245      191. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 245 kwa kufuta matamshi “umri wa miaka kumi na nne iwapo ni mwanaume, au chini ya umri wa miaka kumi na sita iwapo ni mwanamke” na kuyabadilisha kwa maneno “miaka kumi na nane”.
- Marekebisho ya kifungu cha 252      192. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 252 kwa kufuta maneno “kumi na nne” na kuyabadilisha kwa maneno “kumi na nane”.
- Muundo Sura ya 20      (e) *Sehemu Ndogo ya Tano*
- Marekebisho ya kifungu cha 188      193. Sehemu hii ndogo itasomwa kwa pamoja na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, itakayojulikana kama “Sheria Kuu”.
- Marekebisho ya kifungu cha 188      194. Sheria Kuu inarekebishwa katika kifungu cha 188 kwa-
- (a) kukibadilisha kuwa kifungu kidogo cha (1);
  - (b) kuongeza kifungu kidogo kipyga cha (2) kama ifuatavyo:

“(2) Bila kujali kifungu kidogo cha (1), majina na utambulisho wa watoto walio chini ya umri wa miaka kumi na nane vitalindwa”.

*Sheria ya Mtoto*

*Tangazo la Serikali Na. 134 (linaendelea)*

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 70)*

## FOMU YA KUINGIZWA KATIKA REJESTA YA WATOTO WALIO ASILIWA